# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION
# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL , KAITI CONSTITUENCY, HELD AT MUKUYUNI HIGH SCHOOL

## ON

## 9TH OCTOBER 2002

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL OF KAITI CONSTITUENCY HELD AT MUKUYUNI HIGH SCHOOL ON 9TH OCTOBER 2002**

**Present**

1. Com. Abida Ali Aroni

**Secretariat in Attendance**

1. Collins Mukewa - Programme Officer
2. Susan Mutile - Verbatim Recorder
3. Sammy Kiteng'u - District Coordinator

**Meeting started at 11.10 am with Com. Abida Ali in the chair.**

**Sammy Kiteng'u**: Ningumukulya muthengeangie ovaa nundu twi anini. Ekai twambie kyathi kitu kya umunthi na ningumukulya Reverend Solomon Mbunzia atutongoesye na mboya.

**Rev. Solomon Mbunzya**: Ekai tuvoye. Ngai Asa waitu wa ituni ni twooka mbee waku tuikutungia muvea. Twikutungia muvea nundu wa kwithiwa wi Ngai utwendete. Twikutungia muvea nundu wa kwithia ni wendaa maundu methiwe me maseo na Ngai twitunga muvea nundu wa team ila yaendie round na yathi yosaninitye mawoni ma andu undu me kwenda Constitution yitu yithiwe yilye. Ngai niwamatongoisye niwoonie ve kitumi kya kwenda team isu yiiende round, andu maku ni meewie mavinyiwe na mataendee nesa. Na indi Ngai yila kwi thina niwonanasya vinya waku oundu woonanisya kwa ana ma Misili yila mai wungu wa Valao. Ngai nuniinie andu maku miao yila inaikwo itanaile na woona kana ni yaile ku-review-a ni yaile kuandikwa ingi nesa. Ngai ni twatunga muvea nundu wa asu manaendie mosanitye mawoni ma andu na indi ni tweyia mbee waku saani uu kwoondu wa maundu ala tuuthi kunenen'ia yiulu wa uu Ngai ukethiwe vamwe na iitu na ukatutethye. Ngai twina utanu nundu wa wia ula unathukumiwe na Ngai nitukwitikila kana nimathukumie wia museo. Eka indi tukyambiisya wambiisye vamwe na iitu na andu mainengane mawini withiwe vamwe namo. Na indi Ngai ukatutethye na twone ikitikilika na yithiwe ya kutawala nthi yaitu. Mwiai mivango yonthe yila itonya uka nundu wa ala me ivilani ni mewaa mateenda miao ya umavinyiia. Ngai nitwathi ukananisya isyitwani na Yesu Klisto. Uu ni woni wa andu ni woni wa Kenyans na Ngai eke uketikilike, eka waambisye vamwe naitu. Tondu wa ala meethiwa matukwatie kyathi matethye, na eka maundu ala tuunenania twi kwendani kwaku. Na no undu wa isyitwa ya Yesu Klisto nitwavoya. Amen.

**Sammy Kiteng'u:** Asante sana Reverend. Tutaanza mkutano wetu kwa kuwajulisha wale watu wametumwa na Commission kutoka Nairobi na wale tuko hapa. Na nitaanza na mimi, mimi ndio muwakilishi wa Commission katika hii district ama district coordinator. Jina langu naitwa Sammy Kiteng'u na tunafanya kazi tukishirikiana na wale wenzenu wanaitwa 3Cs. Na ninaona hapa kwa siku ya leo tuko na mmoja ambaye ako huko nyuma jina lake ni Beatrice Nzitu. Nitachukua nafasi hii tena nimukaribishe Commissioner wetu kwa hii siku ya leo – Abida Ali Aroni naye atujulishe wale ametoka nao Nairobi halafu tuanze mkutano wetu wa leo. Asante.

**Com. Abida Ali**: Hamjambo? Kama mlivyo elezewa naitwa Abida Ali Aroni Commissioner. Ningependa kuwakaribisha kwa

hiki kikao cha leo na kuwajulisha kwamba nimefuatana na Programme Officer ambaye ni Collins Mukewa na Verbatim Recorder Susan Mutile. Asanteni.

**Sammy Kiteng'u**: Nafikiri tunaweza kuendelea

**Com. Abida Ali**: Katika programme yetu ya leo tunashungulika na mambo yafuatayo. Nitawaeleza kwa kifupi ni kwa nini tumekuja kushirikiana na nyinyi kwa siku ya leo. Halafu kwa vile nyote mnaelewa kisababu ambacho kilitufanya au malengo ya kutuwezesha kufanya marekebisho ya Katiba sitazungumzia hayo maneno. Niwaeleza njia ambazo tulitumia kufikia hadi katika draft Constitution ambayo mko nayo. Halafu kwa kifupi sana nitawapitisha kwenye hiyo draft Constitution na kujaribu kuifananisha au kuitofautisha na Katiba ya wakati huu. Halafu mwisho kabisa nitawapa nafasi ya kuweza kuzungumza kuelezea comments au kuuliza maswali kulingana na hii draft Constitution ili niweze kufafanua ikia kuna jambo ambalo halikueleweka vizuri.

Kisababu cha mkutano huu wa leo ni kuweza kuwaletea rasmi draft Constitution ambayo mmepewa ikiwa amukuweza kupata hapo mbeleni kupitia kwenye magazeti na pia kuwaeleza kwamba hiyo ni draft ya kwanza kutoka kwa Tume na tunatarajia mtaisoma sana na kuangalia kana ina-reflect ama imeweza kutoa mambo ambayo mliweza kutuelezea, na muone kama mngetaka mabadiliko yoyote ikiwa kuna karibu wiki tatu hivi kabla atujaenda katika kikao cha kitaifa, ambapo sasa vikundi tofauti au delegates ambao watakuwa ni zaidi ya mia sita watakao kuja katika hicho kikao cha kitaifa. Wataweza kujadiliana na kuzungumza zaidi kuhusu draft Constitution na hatimaye tuweze kupendekeza Katiba mpya kupitia kwa Bunge. Kwa hivyo ikiwa kuna mambo ambayo mngependa kuyaona yamebadilishwa mtaweza kuwatuma wawakilishi watatu wa district yenu ambao watakuja katika hicho kikao cha kitaifa. Kwa kufikia wakati huu tumepata majina ya wawakili hawa watatu na Bwana coordinator baadaye ataweza kuwaeleza ni akina nani. Mnaweza pia kutuma mapendekezo kupitia kwa Mjumbe wenu ambaye atakuwa mmoja wa delegates ambao watakaa katika hicho kikao cha kitaifa. Lakini ikiwa kuna jambo lolote ambalo ungetaka kusema kwa siku ya leo unaweza lakini uzito mkubwa unatengemea mtakavyo watuma delegates. Kwa sababu sisi tunaweza kuwa na ugumu kwa wakati huu kubadilisha hiyo draft Constitution kwa sababu tumeisabaza sehemu zote za nchi yetu.

Sasa baada ya kuwaeleza hivyo ningetaka kuwajulisha kwamba baada ya kuchukua maoni yenu na maoni ya Wakenya wote kwa muda ambao ulikuwa ni kama miezo sita. Tuliweza kupata watu ambao walichambua maoni na Tume ikaweza kuandika report ambayo ilitusaidia kuweza kujua mambo ambayo mlitueleze. Ripoti hizo tulichapisha na kusabaza kupitia kwenye magazeti na tulitoa tokeo fupi kwa sababu kwa wakati huu bado tunazidi kuandika na kusahihisha tokeo ambalo litakuwa na ukurasa zaidi ya elfu moja ambayo itawaeleza maneno ambayo tulipata baada ya sisi kuzuguka. Na pia pengine Bwana coordinator ataweza kuwapatia hiyo ripoti ambayo ni fupi muendelee kusoma na kulinganisha na hiyo draft Constitution. Pengine ikiwa ana nakala ataweza kuwapatia baada ya mkutano huu.

Sasa baada ya kuandika ripoti hiyo tulijadiliana na kuwaza kuhusu mambo ambayo mlitueleza. Tukajadiliana sana na hatimaye tukaweza kufikia hiyo draft ambayo mko nayo na pia baada ya kusoma maoni yenu pia tuliweza kuangalia mambo tofauti ambayo tuliweza kujadiliana na wataalamu tofauti kutoka Kenya na nchi za ng'ambo kwa sababu kuna mambo mengi ambayo tulitaka kupata mawazo zaidi na tukataka kuzungumza na wataalamu ili watufafanulie zaidi. Kwa hivyo hii draft bill ina maoni yenu na pia ina maoni ambayo tulipata kutoka kwa wataalamu katika mambo tofauti tofauti. Sasa hii draft bill kisheria inatakiwa isabazwe kwa muda wa mwezi na mwezi utakamilika tarehe ishirini na nane wa mwezi huu wa kumi na tunatarajia kwamba kuazia tarehe ishirini na nane ikiwa mambo hayajabadilika tutaweza kuazisha kikao cha kitaifa ili tuweze kujadiliana na tuone kama baada ya hicho kikao mambo yatakuwa vipi.

Sasa tukiingilia hii Draft Constitution ambayo tumewapatia sijui ni watu wangapi wameweza kuisoma kabla ya siku ya leo ndio tuone tutakavyo endelea na kazi. Ni watu wangapi wameiona kupitia kwa magazeti au amesikia kutoka kwa KBC tukizungumzia kuhusu hiyo Katiba? Kuna wale wamesema nina hakika kupitia Nation, Taifa, Standard na the People. Mmeona hii Katiba kabla ya leo? wangapi? Kwa hivyo karibu watu nusu ambao wako hapa. Sasa kwa wale wengine ambao awajaona nafikirikia tutapitia kwa kifupi sana kila chapter ya Katiba hii au pendekezo la Katiba ili niwaeleze kwa kifupi sana ni watu ambao awajasoma pengine wataweza kuwa pamoja na sisi tukijadiliana tukifikia mwisho wa programme.

Kwanza kabisa tuna preamble ama utangulizi ambao tumeupendekeza.. Utangulizi ambao ukiangalia unazungumzia tofauti zetu za kikabila, za kimila, za kidini na pia kuweka mkazo umoja wetu kama wananchi wa Kenya. Na pia imesisitiza umuhimu wa familia katika ujenzi wa taifa na kutambua shughuli ambazo zinafanywa na Wakenya wote ikiwa ni akina mama au wazee. Na pia inatambua kwamba nchi yetu ni nchi huru ambayo ina demokrasia na pia ina sheria ambayo imetusimamia. Inatambua pia umuhimu wetu kama wananchi na haki ambazo tunazo katika utawala wa nchi na hatimaye ikatambua Mwenyezi Mungu. Sasa hapo mtaangalia muone kama kuna mambo tuliwacha, tulipata utagulizi na maoni tofauti lakini tulipokusanya tukaamua kwamba utangulizi huo umeweza kubeba mambo yote, au mambo karibu yote ambayo tulipewa na watu ambao walitoa maoni yao.

Tukitanzama chapter ya kwanza ya Katiba,chapter hiyo inaguzia umuhimu wa wananchi wa Kenya na kuwapa wananchi wa Kenya sehemu yao katika utawala wa nchi na kusema kwamba nguvu zetu kama wananchi wa Kenya kwa serikali zinatakiwa kutumika kulingana na Katika na kwamba nguvu zetu kama wananchi wa Kenya zimepewa mikono minne ya serikali. Tumezungumzia ama kupendekeza kwamba nguvu zetu zimepewa Bunge, zimepewa serikali kuu, zimepewa Mahakama na pia kupewa vyombo ambavyo ni vya Kikatiba.

Halafu tumetambua ukuu wa Katiba katika section two ama kifungu cha pili na kueleza jinsi Katiba hii itaheshimika na watu wote na kwamba ikiwa kuna sheria ama kitendo chochote ambacho ni kinyume cha Katiba hii jambo hilo ama kitendo hicho kitakuwa sio cha halali. Pia tumependekeza jinsi ambavyo tutaweza kulinda na kuhakikisha kwamba Katiba hii ya nchi yetu itafuatwa. Na katika section ya tano tunaeleza kuhusu sheria tofauti za Kenya na tumesema kwamba sheria kuu ni Katiba halafu itafuatiwa na sheria zingine zitazotungwa na Parliament au Bunge. Na baadaye tutakuwa na sheria ambayo ni ya

kitamaduni African Customary Law na kufuatiwa na sheria ambazo zinafuatwa na jamii ya kiislam na wahindu. Baadaye tumesema zitafuatiwa rules ama utaratibu ambao saa ingine kwa sababu umetumika kwa miaka mingi hatimaye huwa ni kama sheria kwa Kiingereza common law. Na pia tukasema kwamba ni lazima tutafuata sheria ambazo zinatungwa na jumuhia ya nchi za Afrika Mashariki East African Community. Tukasema pia ni lazima tufuate sheria ambazo zimetungwa na mataifa yote international law. Na tukapendekeza kwamba kufikia miaka miwili baada ya Katiba hii kutungwa ni lazima Bunge lijaribu kuhakikisha kwamba sheria hizi zote zinaabatana na Katiba ya nchi yetu.

Katika chapter ya pili tunazungumza kuhusu jamhuri ya Kenya na tukasema kwamba kuna maadili fulani ambayo ni lazima hazingatiwe katika jamhuri ya Kenya. Kwa mfano tumesema ni lazima tuwe na utawala mzuri ni lazima tuwe na demokrasia ya vyama vingi na ni lazima tuhusishwe kama wananchi katika utawala wa nchi. Tuwe na uwazi katika kuendesha shughuli za umma. Tuliangalia mji ulio mkuu na tukaangalia lugha ambazo zinafaa kuwa ni lugha rasmi na lugha ya taifa. Na tukabadilisha tukasema baada ya Katiba hii kuundwa lugha rasmi itakuwa ni Kiswahili na Kiingereza, sio Kiingereza peke yake na kwamba Kiswahili kitambakia kikiwa ni lugha ya taifa na serikali itajaribu kukuza lugha zote za jamii ya Kenya. Kwamba ingawa Kiswahili ni lugha ya taifa lakini lugha zingine zitakuzwa ili zisije zikapotea. Halafu tukaangalia dini na serikali na tukapendekeza kwamba serikali ya Kenya isiwe ni serikali ambayo inafuta dini yoyote na tukaweka dini zote ziwe ni za usawa. Na kwamba ikiwa kuna shughuli za kitaifa dini zote zitahusishwa.

Tukaangalia pia vyombo vya kitaifa na tukapendekeza kwamba tuwe na vyombo kadhaa kwa mfano, tukasema kwamba bendera ya Kenya ni chombo cha kitaifa, wimbo wa taifa ni chombo cha kitaifa tukaangalia muhuri rasmi wa serikali tukasema ni chombo cha taifa na tukachukua halama ambayo huwa inawekwa katika vifaa vya mali ya umma ambayo kwa Kiingereza tunaita Court of Arms, tukasema pia hicho ni chombo ambacho ni cha kitaifa ama cha umma. Na tukapendekesa oaths ama kihapa ambacho kitachukuliwa na watu ambao watakuwa wanahudumia au kusimamia kazi muhimu za serikali. Halafu pia tukaangalia siku za kitaifa na tukapendekeza siku fulani tukasema kwamba tunapendekeza kwamba ziwekwe katika Katiba zisije zikawa zinabadilishwa mara kwa mara. Na tumependekeza siku tatu peke yake. Tumependekeza tarehe moja mwezi wa sita kuwa Madaraka day, tarehe kumi na mbili mwezi wa kumi na mbili Jamhuri day na tukasema tuweke tarehe ingine ambayo itajulikana kama Katiba day siku ambayo tutaweza kuwasilisha na kutambua Katiba mpya ya Kenya. Hayo ni mapendekezo mtasoma na kutuambia kama ni sawa ama mngetaka kuongeza ama mupunguza.

Katika chapter ya tatu tunaangalia principles and goals, au maadili ambayo tunathania ni muhimu katika utawala wa nchi yetu na tumetambua vitu kadhaa. Tumetambua uhuru wa wananchi, tumetambua umoja wa taifa letu, tumependekeza usalama na amani, tumependekeza demokrasia na utawala uliyo bora. Tumependekeza haki za kibinadamu, na usawa wa watu wote bila kuwabagua kupitia jinsia au maubile yao na pia bidii inakayotusaidia kuweza kupata mahitaji ya kimsingi kwa binadamu. Tumependekeza kushiriki na uwazi katika shughuli ambazo ni za umma. Tumependekeza uadilifu wa kibinafsi na wa kitaifa, tumependekeza pia kufumilia na kuheshimu maoni ya watu tofauti. Tumependekeza pia kuheshimu mila na maadili tofauti ya Wakenya, kuleta utawala karibu na watu na utatuzi wa mabishano kwa njia ya amani bila kuzozana au kuwa na vita na pia

umataifa na umoja wa Afrika. Hayo ni katika maadili ambayo tumependekeza na mtasoma zaidi ili kuelewa. Katika section ya kumi na tano tumeangalia kuhusu wananchi na tumeangalia majukumu ya wananchi. Katika Katiba yetu ya wakati huu tunaona kwamba sisi kama wananchi hatujapewa jukumu lolote na mara kwa mara huwa tunapiga kelele tukisema serikali haijafanya hivi na hivi lakini atujiangalii na kuona kama sisi tumefanya mambo yanayo kustahili kufanya kama wananchi na pengine ni kwa sababu atujaelezwa.

Sasa kwa wakati huu tumependekeza mambo kadhaa ambayo tunasema ni lazima tuyatende kama wananchi wa Kenya. Kwanza kabisa tumependekeza kwamba kila Mkenya aelewe mambo ambayo yamependekezwa katika Katiba. Tumependekeza pia kila mwananchi aweze kusimamia na kutetea Katiba ya nchi yetu na kwamba kila mwananchi alazimike kupiga kura na kuzihuisisha na siasa za nchi. Na hii tumependekeza kwa sababu mara kwa mara watu huwa hawataki kupiga kura wanajiandikisha na siku ya kura awaendi na baadaye tunalalamika atumpendi huyu kiongozi, atupendi viongozi lakini hatutaki kijiuzisha na kupiga kura na siasa za nchi.

Pia tumependekeza kwamba kila Mkenya aweze kujibidiidha katika kazi yake na kuweza kuwa na familia na kuangalia hiyo familia kwa sababu chanzo cha taifa kizuri ni familia iliyo bora. Na pia tukapendekeza kwamba kila mwananchi aweze kujielimisha awezavyo mara kwa mara ili tuweze kuwa na maendeleo ambayo ni bora. Na kwamba sisi sote ni lazima tuchangie maendeleo katika jamii zetu. Na pia tumependekeza ni lazima sisi sote kama wananchi tuweke bidii ili tuwe na umoja kama taifa la Kenya na tuishi kwa njia ya amani. Na pia tumependekeza kwamba kila Mkenya ni lazima akuze demokrasia ua tabia za kidemokrasia na kuweza kuheshimu sheria za nchi. Tumependekeza kwamba ni jukumu la kila mwananchi kuchunga mali ya umma bila kuiharibu. Kwa mfano liwe ni jukumu la kila mwananchi kuchunga mito, milima, buga, wanyama wa pori kwa sababu hiyo ni mali ya nchi yetu. Na kwamba sisi kama wananchi pia tujihepushe na rushwa. Tunalalamika kwamba wafanyikazi wa serikali wanachukua hongo na rushwa lakini tunasahau kwamba sisi ndio tunawapatia hiyo hongo na rushwa sasa tunasema tuwajibike kana wananchi wa Kenya kutokujiuzisha na vitendo ambavyo havifai. Pia tuweze kukuza sehemu ya Kenya katika ulimwengu.

Halafu pia tukatizama ni nani ambaye anaweza kuwa ni mwananchi wa Kenya na tukapendekeza kwamba mwananchi wa Kenya awe ni mtu ambaye atakuwa amezaliwa Kenya kupitia mzazi mmoja ambaye ni Mkenya awe ni mzazi wa kike ama wa kiume. Na pia watu ambao wataweza kujiandikisha kupitia sheria ambazo zitawekwa na Bunge. Jambo lingine ambalo pengine mngependa kuangalia ni kwamba tumependekeza kwamba raia wa Kenya waweze kuwa na uraia wa nchi nyingine ikiwa mtu angependa kufanya hivyo.

Katika ukurasa ufuatao ambao ni wa tano na ambao ni muhimu kwa maisha yetu kama wananchi wa Kenya ni inazungumzia haki za kimsingi ama haki za kibinadamu. Ingawa Katiba ya wakati huu imetupatia haki za kimsingi wakati ambapo tulikuwa tunachukua maoni tulielezewa kwamba haki hizo hazikutosha na tukaelezewa kwamba inafaa tuzipanue ziwe nyingi zaidi. Na kwa wakati huu utaona kwamba chapter hii ni ndefu zaidi. Kutoka section ya ishirini na tisa hadi ya sabini na tano

tunazungumzia kuhusu haki za kimsingi. Na haki hizi zinaanza kwa kusema kwamba demokrasia ndio chanzo cha haki za kimsingi, haki za kijamii, haki za kitamaduni na haki za kiuchumi. Na sasa tumepewa haki na serikali italazimika kuchunga, kuheshimu na kukuza haki ambazo tumesema ni za kimsingi. Ingawa sote tumepewa haki hizi lakini hizi haki zinaweza kunyimwa wakati ambapo italazimika ikiwa mtu ambaye anajaribu kutumia hiyo haki atakuwa anamdhuru mwenzake ama kufanya kitendo ambacho pengine kitakuwa akifai. Na katika haki ambazo tumepewa ni haki ya maisha, right to life na kwa sababu tumetoa haki ama tumependekeza haki ya kimaisha tumependekeza kwamba death penalty ama hukumu ya kifo iondolewe. Pia tumependekeza kwamba kuwe na usawa mbele ya sheria usawa ambao utatolewa kwa wananchi wote bila kuwabagua na tumesema kwamba hizi haki za kimsingi sitolewe pia bila ubaguzi kwa kila Mkenya.

Tumependekeza kwamba Mkenya yeyote asiwe anabaguliwa kupitia kabila lake, umbo lake au sehemu yake katika jamii. Asibaguliwe kwa sababu ya umri wake au kwa sababu ya dini au maubile au lugha au kwa sababu ni mlemavu. Pia kukatolewa haki za wanawake kwa sababu katika Katiba tuliyo nayo sasa aijatofautisha haki. Na tulipokuwa tunachukua maoni akina mamì¥ÁM ð ¿ Mbjbjâ=â= "´?W?W Ù Œ sÿÿ ÿÿ ÿÿ l > ¦#¦#¦#8Þ# ì¥ÁM ð ¿ Mbjbjâ=â= "´?W?W Ù Œ sÿÿ ÿÿ ÿÿ l > ¦#¦#¦#8Þ kama wanavyopewa wanaume. Pia tumependekeza kwamba akina mama wasibaguliwe wakati wa kurithi mali wawe na usawa na wanaume na waweze kupata mali na kumiliki mali bila ubaguzi wowote. Pia tukapendekeza kwamba kusiwe na sheria yeyote hata ikiwa ni sheria ya kimila itakayotumika kunyanyaza na kubagua akina mama. Na hii tukapendekeza kwamba serikali itambue sehemu ya akina mama wakiwa ni wazazi katika jamii na kuweza kuwapatia vifaa na usaidizi utakaoweza akina mama kuendeleza maendeleo yao katika jamii. Na pia wapewe haki za elimu, haki za kushiriki katika ofisi tofauti za kiserikali.

Na pia tumeangalia haki za watu ambao ni wazee katika jamii na tukaeleza kwamba watu hawa wapewe nafasi ya kujishungulisha na mambo ambayo ni ya kijamii, wapewe nafasi ambayo wanaweza kujiendelesha mambo yao. Wasitukanwe na kubaguliwa na wapewe heshima na waweze kuangaliwa ipasavyo na jamii zao na pale jamii haiwezi serikali iingie na kusaidia hawa watu ambao ni wazee.

Halafu pia tukapendekeza haki ambazo tunasema ni haki za watoto. Kwenye Katiba ya wakati huu haina haki za watu waze na pia haina haki ya watoto. Na katika pendekezo letu tumesema kwamba ni lazima tutambue sehemu muhimu ambayo ni ya watoto katika jamii yetu. Na tukapendekeza kwamba ni jukumu la wazazi, jukumu la jamii kama vile wajomba na nadhalika na jamii communities ama societies kuwachunga, kuwaelimisha na kulea watoto kwa njia ambayo inafaa na kuwapa mapenzi, kuwapa heshima na kuwapa furaha kwa njia ambayo wanakuzwa bila kuwasumbua na bila kuwanyima nafasi ya wao kuweza kukua kwa njia iliyo bora. Na kwamba watoto watakao zaliwa nje au ndani ya ndoa waweze wote kuangaliwa ni kama wako sawa na wazazi wakiwa wameoana ama awajaoana waweze kuwachunga watoto hawa kwa njia ambayo inafaa. Na kwamba kila mtoto ni lazima apewe jina la familia, ni lazima awe na uraia, ni lazima awe na haki ya kulelewa na wazazi hata ikiwa wametengana ama awajaoana. Na kila mtoto ni lazima apate elimu ya kimsingi ya lazima na ya bure. Na kwamba watoto wachungwe na tuone kwamba awatapewa kazi ambazo azifai kupewa watoto, wasibaguliwe na pia wasipewe kazi ngumu ama

viboko kama njia ya kuwaadhibu ama kwa kuwapatia nidhamu. Na kwamba watoto wasiwe wanashikwa kupelekwa gerezani ila ikiwa hakuna njia yoyote ya kuweza kumsaidia huyo mtoto. Na akishikwa serikali iweze kutoa utetezi ama kutoa wakili atakaye simamia huyu mtoto na kumtetea. Na kwamba watoto ambao hawajiwezo kwa mfano watoto ambao ni mayatima wasio na wazazi, watoto ambao pengine ni walemavu, watoto ambao awana makao mahalum waweze kuchungwa na jamii na serikali. Na kwamba kulingana na sheria mtoto tunapendekeza awe ni mtoto ambaye ana chini ya miaka kumi na minane.

Halafu pia tukaangalia familia kwa sababu tunasema familia ndio msingi katika jamii tukasema kwacha tuangalie kisheria familia ni ngani na tukapendekeza mtaweza kusoma na kuelewa hapo. Na pia tukaangalia watu walemavu ni akina nani na katika kifungu thelathini na tisa tumewaelezea watu ambao ni walemavu na tukaweza kufafanua na kuongozea watu ambao kawaida usemekana ni watu walemavu. Na kwa sababu jambo hili lilizungumziwa sana kwa kifupi nitawaelezea jinsi Katiba mpya inawatambua watu ambao ni walemavu. Tumesema na kupendekeza kwamba kusiwe na ubaguzi katika haki za kimsingi za watu ambao ni walemavu. Tumeongezea kusema kwamba watu ambao ni feru feru ama ni slow katika kufirkiria na watu walio na firusi vya Ukimwi pia waangaliwe ni kama watu walemavu. Na tukapendekeza kwamba watu ambao ni walemavu wapewe nafani ya kuweza kuoa na kuwa na familia kama watu wa kawaida. Na kwamba wawe na haki ya kuwakilishwa katika viwango vyote vya utawala, na kwamba serikali iweze kutumia lugha ambayo inaeleweka kwa watu walemavu kwa mfano, lugha ya ishara na Braille. Na kwamba mahitaji ya watoto walemavu yaangaliwe. Na kwamba serikali iwe na jukumu la kuona kwamba majengo na njia za kusafiri na mawasiliano zitaweza kuwafikia watu ambao ni walemavu.

Pia katika hii chapter ya haki za kimsingi tumezungumzia kuhuru haki ya kisiasa katika Article ya hamsini. Tumezungumzia kuhusu haki za wafanyikazi katika Article ya hamsini na tatu. Tumezungumzia elimu, nyumba, chakula, maji na pia tumezungumzia kuhusu haki za ununuzi na haki ya huduma ambapo utakuwa umetoa pesa zako na kutaka kuhudumiwa, haki ya kuweza kufikia mahakama kwa njia iliyo sawa na rahisi. Na pia haki ya kuweza kuende kortini ili kuhakikisha kwamba haki zako za kibinadamu zimetolewa bila shida yoyote.

Katika chapter ya sita tumezungumzia kuhusu haki za kuwakilishwa kupitia katika kura. Na hapa tumependekeza jinsi ambavyo tutaweza kufanya shughuli zetu za uchaguzi na tukasema kwamba kupiga kura ni haki ya kila Mkenya na tuweze kupiga kura ambazo ni za siri, kura ambazo ni za haki na za halali, kura ambazo zitaweza kutoa, kutekeleza wanavyo taka wananchi. Na kwamba katika upigaji wa kura tutaweza kuwapa walemavu akina mama na jamii ambazo zimetegwa nafasi yao. Na kwamba kura hizo zimeweza kusimamiwa na Tume ambayo iko huru ambayo haiwezi kuingiliwa kisiasa na pande yoyote. Na tukaangalia haki ya kupiga kura tunaambiwa kila Mkenya ambaye ana zaidi ya umri wa kumi na nane ana haki ya kupiga kura. Tumependekeza ni kina nani ambao wataandikishwa, kina nani ambao watakosa kuandikishwa na pia tumependekeza kwamba uandikishaji uwe ni jambo ambalo linaendelea kila wakati bila kusumbiri wakati wa kupiga kura. Na tumependekeza katika Article ya thamanine na tatu kwamba kuwe na tume ya kusimamia kura na tumependekeza kwamba ingawa wakati huu Tume hiyo ina watu ishirini na wawili kwamba wapuguzwe wawe ni watu nane wakizidi sana wawe ni watu kumi. Halafu tumeopendekeza jinsi watakavyo chaguliwa hapo mtasoma.

Na tumependekeza kwamba watakuwa wanaandikisha wapiga kura kila wakati, na kwamba wataangalia boundaries za Constituencies, wataweza kusimamia kura, wataweza kuhakisha kwamba hizo kura zitakuwa ni za halali. Watakuwa ni wasimamizi wa vyama vya kisiasa na pia watakuwa ni wasimamizi wa pesa zitazotolewa na serikali kwa vyama vya siasa. Watakuwa pia wanasuluhisha mizozo iatakayo tokana kwenye upigaji wa kura na pia watasomesha watu elimu ya upigani wa kura na kutueleza zaidi kuhusu msimamo wa demokrasia. Na kwamba watakuwa ni chombo huru wakati wa kufanya kazi zake. Mtasoma kuona jinsi ambavyo waandikisha vyama vya kisiasa na vile wataweza kusimamia hizo pesa zitakazo tolewa na serikali lakini tumependekeza kwamba pesa ambazo zitatolewa kwa vyama vya kisiasa visizidi point tatu ya asilimia ya budget ya nchi yetu. Na kwamba asilimia hamsini zitangawiwa vyama ambavyo vitapata 5% ya kura zitazokuwa zimepigwa katika nchi yetu na hivyo vyama vimewakilishwa Bungeni. Lakini asilimia hamsini itakayopewa italingana na Wajumbe ambao watakuwa wamepelekwa Bungeni na chama chochote kile.

Halafu chapter ya saba tumeangalia katika ukurasa au Article mia moja na moja kuhusu Bunge. Na tumependekeza kwamba Bunge ya nchi yetu kwa wakati ujao iwe kwa mara mbili wakati huu tuna Bunge moja. Tumependekeza kwamba tuwe na National Council ambayo kwa jina lingine unaweza kuita Upper House ama Senate na tuwe na National Assembly ambayo itakuwa ni Lower House. Na tumependekeza kwamba watu watakao chaguliwa katika Upper House ama National Council watoke katika wilaya tofauti. Na tumetambua wilaya sabini na tunapendekeza kwamba watu hawa wachaguliwe kutoka hizo wilaya sabini ingawaje tumesema itakuwa na Wabunge mia moja na kwamba wale thelathini wawe ni akina mama kwa sababu kawaida akina mama awawezi kubishana ama kung'ang'ania viti kama wanavyo ng'ang'ania waunaume na tukasema akina mama hawa watoke katika province. Kwa sababu tuna province saba ukiondoa Nairobi. Na tunapendekeza kwamba kila province itoe akina mama wanne ambao watapigiwa kura na Nairobi ipewe akina mama wawili. Na hawa watapigiwa kura baada ya kujitokeza.

Halafu pendekezo letu la Lower House au National Assembly ni kwamba kuwe na members ambao ni mia tatu. Mia mbili na kumi watachaguliwe kama ilivyo kawaida. Waje katika Constituency ishirini na kumi na wachaguliwe. Tunapendekeza kwamba wale waliobakia tisaini wachaguliwe kwa kupitia orodha itakayo tolewa na vyama. Na tulipendekeza hivi kwa sababu watu wengi walilalamika kuhusu Wabunge ambao wanateuliwa na wakasema kwamba Wabunge hawa ambao wanateuliwa kawaida huwa ni marafiki ama watu ambao wanachaguliwa na Rais kwa kupitia mambo tafauti. Na tukapendekeza kwamba watu hawa wawe wanachaguliwa kupitia vyama vya kisiasa. Na tunapendekeza kwamba vyama vya kisiasa viangalie mambo tofauti kwa mfano, viangalie watu wa jamii ambazo pengine zimetegwa magionalist, waangalie watu ambao ni walemavu, waangalie vijana na waangalie kwamba watu wote nchini wameweza kufika katika Bunge. Na kila chama kitatakiwa kitoe orodha ya majina kulingana na watu ambao wangetaka first come in the list. Kwamba ni nani katika hiyo list wangependekeza zaidi aende katika Bunge na hiyo orodha yao ikiwa number moja ni mama wapili awe ni mwanaume mpaka watapofikisha number ambayo watakuwa wameelewa kwa sababu ilitalingana na kura ambazo kila chama kitakuwa kimepata Bungeni.

Halafu katika ukurasa huo ukurasa tumeweza kueleza kazi ambazo zitafanywa na Bunge na tumeweza kuongeza kazi ya Bunge. Tumesema kwamba Bunge itakuwa inatengeza sheria tofauti za nchi yetu lakini pia tukasema kwamba Bunge itakuwa na mambo mengine zaidi ambayo yatawezesha kuendesha mambo ya kiserikali sawasawa. Kwamba Rais na Waziri Mkuu watapaswa mara kwa mara kuzungumza na Bunge ili wapewe idhini ya kufanya mambo fulani. Kwa mfano Rais ni lazima ajadiliane na Buge katika kuteuwa Waziri Mkuu naye Waziri Mkuu ni lazima kuzungumza na Bunge ili kuweza kuteuwa Mawaziri na naibu wa Mawaziri. Pia Bunge imeshurutihswa kutengeneza budget na kuhakisha kwamba budget ya nchi inatumika kwa njia iliyo bora. Na kwamba Bunge litahusiswa kwa mfano wakati ambapo Rais angetaka kuweka hali ya hatari ama kutambua kwamba nchi yetu itaingia kwenye vita na nchi zingine. Bunge pia itaweza kupitisha kutokuwa na imani na Prime Minister ama Waziri Mkuu inaweza pia kupendekeza kwa kuondolewa kwa Rasi kwa sababu amekosa kufanya mambo ambayo anasitahili kufanya kama Rais. Pia Bunge litatakiwa kuwa na Tume tofauti zitakazo Bunge kufanya kazi zake. Nafikiria mtaendelea kusoma kwa sababu Bunge imepewa kazi nyingi zaidi na kila mkisoma mtaweza kuelewa kazi ambazo zimepewa Bunge kwa wakati huu.

Halafu tukaangalia katika chapter itakayo fuata tunaangalia Executive ambayo ni serikali kuu na tumependekeza kwamba katika Executive tuwe na Rais, Waziri Mkuu na Baraza la Mawaziri. Tumependekeza kwamba Rais achaguliwe na wananchi na awe ni mtu ambaye atapata kura asilimia hamsini na moja ya kura zote zitazokuwa zimepigwa. Na kwamba Rais wakati atakuwa anagombea kiti hicho asimame na mtu ambaye huyu Rais akishinda atakuwa ndiye Makamu wa Rais na mtu huyu atakaye simama na Rais asiwe ni mtu hovyo hovyo lakini mtu ambaye anaweza kujisimamia kama Rais. Atapita mitihani yote ambaye tumeweka ya Rais. Na kwamba Rais aweni mtu ambaye amesoma na kupata shahada ya degree. Na kwamba Rais awe anafanya kazi kwa miaka mitano na anaweza kurudi kwa mara mbili peke yake na sio zaidi. Na chini ya Rais kutakuwa na Waziri Mku ambaye atakuwa amechaguliwa na Bunge baada ya jina lake kupendekezwa na Rais. Na ikiwa Rais amependekeza jina la Waziri Mkuu na Bunge likakataa basi ataweza kupendekezwa na Mkuu wa upizani. Na ikiwa mtu ambaye amependekezwa na mkuu wa upinzani amekataliwa na Bunge basi Rais ataweza kutambua jina la mtu mwengine yoyote ambaye ni Mbunge na kwamba pia Waziri Mkuu tumependekeza awe kwanza kabisa akitambuliwa na Rais awe ni kiongozi wa chama ambacho kina viti vingi katika Bunge. Na tumependekeza kwamba Mawaziri wasizidi kumi na tano na ikiwezekana wachaguliwe nje ya Bunge na wawe na manaibu pia wasio pungua kumi na watano. Mtaweza kuangalia kazi ambazo amepewa Rais katika kifungu mia moja na hamsini na moja 151 imetueleza kazi ambazo Rais amepewa kufanya.

Tumependekeza kwamba Rais atafungua na kuhutubia Parliament au Bunge kila wakati ambapo itakuwa inaazishwa na kwamba atahudhuria Bunge rasmi mara moja kwa mwaka na pia anaweza akipenda kuhidhuria Bunge mara kwa mara. Na kwamba anaweza kuvunja Bunge kupitia kifungu mia moja arobaini na mbili ambacho kinasema kwamba Bunge linatafunja kulingana na tarehe yake. Kwa hivyo Rais hatakuwa huru tena kuvunja Bunge atakavyo. Na kwamba ataweza kuteuwa watu fulani kwa mfano, atateuwa Waziri Mkuu lakini kama tulivyosema atateuwa baada ya kuzungumza na kukumbaliana na Bunge. Atateuwa Naibu wawili wa Prime Minister kupitia njia hiyo hiyo. Ataweza pia kuwateuwa Mawaziri na manaibu wa Waziri pia

kupitia Bunge kama tulivyoseme. Ataweza ku-appoint Judicial officers kupitia sheria itakayokuwa imekwa ambayo ni kwamba atapitia Judicial Service Commission. Na kwamba kupitia idhini ya Baraza la Mawaziri ataweza kuteuwa tusome kwa sauti na kupitia idhini hiyo ya Baraza la Mawaziri ataweza kuidhiniswa miktaba tofauti ya kitaifa. Na pia kama nilivyo waambia kupitia Baraza la Mawaziri kupitia Bunge na kupitia kikao maalum cha utawala, ataweza kutueleza wakati ambapo tutakuwa katika hali ya vita ama ya hatari. Na pia anaweza kufanya mambo yafuatayo sio lazima kuwateuwa Ma-ambassadors, kuwakaribisha Ambassordor wa nchi za nje. Akipenda pia anaweza kuomba korti kuu itakayoitwa Supreme Court kumpatia mawaidha kuhusu mambo tofauti ya Kikatiba. Anaweza kusamehe wahalifu na anaweza baada ya kuzungumza na kujadiliana na Waziri Mkuu kutoa heshima za kitaifa kwa watu tofauti. Na anasulutishwa na Katiba kuweza kuidhinisha mambo yote ambayo Kenya imekubaliana na nchi zingine kuidhinishwa Kenya.

Na kulingana na shughuli za kibunge anasemekana kwamba Rais anaweza kuazisha mswada wowote kwa Bunge kupitia Baraza la Mawaziri. Na kwamba mswada wowote ukipitishwa na Bunge na kuletwa kwa Rais anaweza kuhihisha bila kusema chochote, anaweza kukosa kuisahisha na kuomba korti kuu kumpatia mawaidha na maoni yake ama anaweza kuirudisha Bunge na kusema isahihiswe.

Sasa pengine tuangalie kazi za Waziri Mkuu ni zipi. Ukiangalia ukurasa mia moja na sabini tunaambiwa kwamba Waziri Mkuu ndiye atakuwa msimamizi wa Baraza la Mawaziri na ndiye atakayekuwa chairman wa mikutano hiyo. Na kwamba yeye na Mawaziri ndio watakao simamia shughuli za kiserikali. Na kwamba Waziri Mkuu ndiye atakayeweza kutengeza budget na kusimamia na kuhakikisha kwamba budget hiyo ama kisio la pesa za nchi zinatumika vilivyo. Ndiye ataazisha miswada ambayo ni ya kiserikali katika korti na ndiye atasimamia na kuhakikisha kwamba maagizo yote yatafuatwa, ndiye atakuwa msimamizi wa mashirika yote ya kiserikali na Ministry zote. Na ndiye atakuwa msimamizi wa shughuli zote za kiserikali hila zile ambazo zimepewa President. Sasa hizo ndizo shughuli za Prime Minister. Mtasoma zaidi na kuzilinganisha na shughuli za Rais na kuona kama ziko sawa sawa ama mna maoni tofauti.

Katika chapter ya tisa tumefanya mapendekezo kuhusu mahakama na uendeshaji wa sheria katika nchi yetu. Tumependekeza kwamba tuwe na korti mpya ya juu zaidi ambayo itaitwa Supreme Court ambayo itasimamiwa na ma-judge wapya sio wale ambao wako kwa wakati huu. Tumependekeza kwamba baada ya hiyo Supreme Court tuwe na mahakama ya rufani ama Court of Appeal, tukitoka hapo tuwe na mahakama kuu High court na chini tuwe na Magistrates courts. Kwa hivyo pendekezo ni kwamba juu ya korti ambazo tuko nazo sasa tuwe na korti ya juu zaidi.

Pia tumependekeza jinsi ambavyo ma-judge wataweza kuteuliwa katika ukurasa wa mia moja tisini na nne 194 na pia 195 tumezidi kueleza ni akina nani wataweza kuteuliwa kuwa ni ma-judge na imeendelea hadi 202, tumeeleza ni akina nani wengine wataweza kuwa wafanyikazi wa kortini. Tumeeleza kwamba Tume inayosimamia shughuli za mahakama iongezewe nguvu ili kuweza kulinda masilahi ya wananchi na kuweza kutunza na kuifadhi umuhimu wa hiki chombo cha serikali mambo hayo yako katika Article 204. Na tukasema watu watakao kaa pale wasiwe tu ni watu wakuu katika serikali na ma-judge ambao

wakiambiwa waangalia ma-judge wenzao watakuwa na ugumu fulani. Na tukasema wananchi wa kawaida pia wahusiswe katika Judicial Service Commission na tukawapatia Judicial Service Commission kazi nyingi zaidi ili kuweza kuifadhi na kukuza chombo hicho cha utawala. Na tukasema kwamba ikiwa judge atatolewa Judicial Service Commission au Tume hiyo ya Mahakama iweze kupendekeza kwa Rais kuwazisha korti maalumu tribunal itakayoweza kufanya upelelezi na kuona kama judge huyo ana makosa ili aweze kuondolewa. Na pia tukaeleza kwamba vile ambavyo Judicial officers watakavyo staafu na pia tumeeleza jinsi ambavyo mishahara yao itavyo lipwa na kwamba Tume itakayo undwa itakayo kuwa inaangalia mishahara ya wafanyikazi wakuu wa serikali pia izishughulishe na mishahara ya ma-judge. Na pia katika utawala wa sheria tumependekeza kwamba ofisi ya mkuu wa sheria ingawanishwe mara mbili. Kwa sababu tulipata malalamishi kwamba mkuu wa sheria ndiye mkuu wa kupendekeza mambo ya kisheria kwa serikali na pia ndiye mkuu wa mashtaka. Sasa pale inakuwa kazi zake zinagongana na tukapendekeza kwamba mkuu wa sheria abaki akiwa ndiye legal adviser, mkuu wa serikali lakini kuwe na afisa mwengine atakaye kuwa ni mtetezi wa kesi za serikali atakayeitwa Director of Public Prosecution. Kwa wakati huu kuna Director wa Public Prosecution ambaye ni kama number tatu kutoka kwa mkuu wa sheria na anafanya kazi kupitia utaratibu unao wekwa na Mkuu wa sheria. Tumesema awe huru na awe na anajisimamia.

Pia tukapendekeza kwamba kuwe na mtu atakayesimamia ambaye tutamwita mtetezi wa haki za wananchi ama Public Defender ama kwa lugha nyingine Ombudsman ambaye ataweza kusimama na kutetea haki za wananchi. Mtu ambaye wananchi wanaweza kuenda kwake bila kuwa na wasi wasi kushtaì¥ÁM ð ¿ Mbjbjâ=â= "´?W? WÙŒ sÿÿ ÿÿ ÿÿ l > ¦#¦#¦#8Þ# ì¥ÁM ð ¿ Mbjbjâ=â= "´?W? WÙŒ sÿÿ ÿÿ ÿÿ l > ¦#¦#¦Katiba. Na kwamba katika shughuli zao za kikazi ni lazima wawe waaminifu na waweze kuangalia masilahi ya wateja wao kwa njia inayostahili. Na kwamba wakili ni lazima akisimama mbele ya korti au mahakama ya aina yoyote kuweka haja ama masilahi ya mteja wake mbele. Na pia ni kazi ya wakili kusaidia korti zote kuweza kutoa hukumu iliyostahili. Na kwamba ataweza kutoa maandiko ua chochote kile kitaweza kusaidia korti mbali na kutoa siri za mteja wake kwa korti. Kwa sababu katika kihapo cha mawakili wanasema kwamba hawezi kutoa siri ya mteja wake wala hawawezi kulazimishwa. Lakini sasa Katiba inasema ikiwa una jambo ambalo unalijua ama una kitu ambacho kitasaidia mahakama na vitu hivyo haviwezi kumdhuru mteja wako ni lazima uvitoe ili mahakama iweze kutoa hukumu ambayo itafaa.

Tukiingilia chapter ya kumi tunaangalia utawala na jinsi utawala huo unangawanyishwa. Katika mapendekezo yetu tumesema kwamba kwa upande wa chini katika muundo wa serikali tungetaka kuwa na serikali itakayofika vijijini na kwamba hii serikali itatimiza malengo yafuatayo. Kwamba serikali itaweza kuwapa watu utawala ulio bora utawala utakao wahusisha kama wananchi wa Kenya. Kwamba utawala huu utaweza kuunganisha jamii tofauti za Kenya. Utawala huu utaweza kuhakisha kwamba kuna demokrasia na uwazi katika kueneza huo utawala kwamba vyombo vyoe vya serikali vitakuwa huru kufanya kazi yake na kwamba vyombo hivyo vya serikali vitaweza kukuza hali ya kijamii na kutuwezesha kuwa na maendeleo ya kiuchumi. Kwamba pia katika utawala huo tuwaweza kungawa rasilmali na mali zingine za umma kwa njia ya usawa tukiweka maanani kwamba kuna sehemu zingine za nchi yetu ambazo zinafaa kuangaliwa zaidi. Na kwamba utawala utaweza kuwezesha

utawala kuwafikia wananchi mpaka katika mashinani. Na kwamba utawala utaweza kuwahudumia wananchi kwa njia nzuri na iliyofaa na kwa njia ambayo sio ya asara. Na kwamba utawala utaweza kukuza haki na matakwa ya jamii zilizotegwa na watu wasio jiweza.

Na katika kuweza kusabaza utawala hadi mashinani tumependekeza utawala kwa njia ufuatayo. Kwanza kabisa tuwe na utawala katika vijiji na tunasema tuwe na village council. Village Council hii itakuwa inatawala kupitia wazee wa vijiji au ikiwa watu wa kijiji wanaona wale wazee hawafai wataweza kupiga kura ili wawe na watawala wa vijijini. Na watu hao watakao tawala katika kijiji sasa haitakuwa ni mtu mmoja kama chief tunapendekeza wawe sita ikizidi wasifike kumi between six and ten. Na kwamba watu hawa wenyewe watajiamlia jinsi wangetaka utawala uwe bila kupewa masharti au muongozo kutoka nje. Halafu kutoka katika vijiji tunapendekeza tuwe na serikali ya councils au locational government au locational council na watakao tawala pale watakuwa ni watu kutoka katika vijiji vya location hiyo. Na kila kijiji kitatoa wawakilishi wawili na tumependeza kwamba katika hawa wawakilishi wawili ni lazima mmoja awe ni mama. Lakini vijiji vikitaka kutoa wamama wawili sheria aijakataa. Lakini lazima mmoja awe ni mama na kwamba serikali hii ya kata ndio itakuwa na uwezo mkubwa wa utawala ambao utatawala location hiyo na wataweza kuandika mtu atakaye kuwa ni administrator ama msimamizi wa shughuli za council hiyo.

Halafu tukitoka katika location tumependekeza utawala uende kwa district level na kuwe na District Council na kwamba watakao kuwa katika hiyo District Council watachaguliwa. Watakuwa watu baina ya ishirini na thelathini kutengemea kila district watakavyoona ni sawa. Na watachaguliwa kupitia kura na wakaazi wa district hiyo. Na pia hawa wataweza kuwa na adminstrator ambaye atachaguliwa pia na wananchi.

Haya tukutoka katika district tunapendekeza sasa tuwe na Provincial Council ama Provincial Government na watu ambao watakuwa katika Provincial Government watakuwa wameteuliwa kutoka katika district. Na kila district katika hiyu province itateuwa watu wawili mmoja ambaye ni lazima hawe ni mama. Na mkisoma katika schedule ambazo ziko kule nyuma sijui ni schedule ngapi, tumewaeleza kazi zitakazo fanywa na hizo serikali za mashinani. Nafikiri schedule seven, tumeeleza National Government itafanya kazi ngani, District Government pia itafanya kazi ngani. Mkisoma mtaona kazi zote ambazo zitafanyika. Na katika section ya mia mbili na ishirini tumetoa functions pia ambazo zitafanywa na Provincial Council katika usaidizi wake wa shughuli za province hiyo.

Chapter kumi na moja tunazungumzia kuhusu mashamba na mali land and property rights ardhi na mali tofauti. ---- na watu tofauti, watu binafsi, jamii au jumuia. Na tumependekeza kwamba mtu asiye Mkenya asiwe na haki ya miliki ardhi hapa nchini. Pia tumependekeza kuteuliwe Tume itakayosimamia shughuli za ardhi ili Tume hiyo iweze kuchuga ardhi au mali ambayo ni ya umma na kuhakisha kwamba ardhi hiyo inatumika kwa njia ambayo inafaa. Pia tumefafanua zaidi maana ya ardhi ambayo ni ya umma na tumependekeza kwamba ardhi ambaye ni ya mtu binafsi mtu huyu aweze kumiliki ardhi hiyo bila kuingiliwa na serikali, na ikiwa serikali inalazimika kuchukua ardhi ya mtu iweze kumlipa kwa njia ambayo inastahili. Na kwamba umilikaji

wa ardhi uweze kulindwa na sheria bila ubaguzi na Mkenya yoyote bila ubaguzi wa iana yoyote aweze kumiliki ardhi katika sehemu yoyote ya nchi yetu. Pia tumependekeza kwamba kupitia miaka miwili baada ya kutungwa kwa hii Katiba Bunge itoe sheria ambayo itafanya mambo yafuatayo. Sheria ambayo itaweza kujumuisha kanunu ambazo nimezungumzia na pia sheria itakayo weza kutatua mizozo ya ardhi kwa sababu tuna mizozo tofauti na sheria zilizoko kwa wakati huu zimeshidwa kutatua mizozo hiyo. Pia tumependekeza kuundwe mfumo wa haraka utakayo saidia ungawanyishiji wa ardhi uwe sio wa garama ya juu, uwe umerahisiswa upande wa bei na utaratibu ili mwananchi wa kawaida asiwe na taabu wakati wa ungawanyaji wa mali. Pia kuwe na ungawanyaji wa ardhi kwa njia ya uhaki na kutatuliwe matatizo ya watu wasio na ardhi. Na pia kuchuguza na kutatua madai ya kihistoria hasa madai ambayo yamewekwa na wakaazi wa mkoa wa pwani. Wakaazi wa mkoa wa kasikazini mashariki na wakaazi wa bonde la ufa au Rift valley na sehemu zingine za Kenya ambapo watu wameteta sana kuhusu mambo tofauti ya ardhi.

Na pia waangalie jinsi tutaweza kodi kwa ardhi isiyotumika na ile isiyo tumika kikamilifu. Sasa hayo ndiyo mambo ambayo tumependekeza kuhusu ardhi. Pia tumependekeza mambo tofauti katika chapter twelve kuhusu mazigara na mali ya asili na jinsi serikali na mwananchi wa kawaida tunaweza kushirikiana na kuweza kuchuga vifaa hivyo.

Katika chapter ya kumi na tatu tumezungumzia pesa za umma na kodi ambazo zinapatikana na tukaeleza kwa kirefu jinsi ambavyo Bunge litaweza kuzihuzisha na kuchuga pesa hizi ambazo ni za umma na kwamba matumizi yoyote ni lazima yawe ni yale ambayo yalipitishwa kupitia Bunge. Pia Bunge lihusishwe wakati ambapo serikali ingeteka kuchukua deni. Tumeelezea pia kazi na shughuli za Banki Kuu. Na pia tukangawa ile ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa fedha za umma tukasema tuwe sasa badala ya kuwa na Controller and Auditor General tuwe na watu wawili tofauti. Tuwe na Controller of Budget Msimamizi wa bageti ama makisio ya fedha za umma. Tukasema mtu huyu awe na kazi ya kuhakikisha kwamba pesa zitazo pitishwa ziwe ni zile zilisoitishwa na Bunge. Na Auditor General awe kazi yake ni kutizama hesabu na matumizi ya pesa na umma.

Halafu katika chapter ya kumi na nne tumeangalia huduma za usalama. Na tukapendekeza kwamba vyombo vya huduma vya usalama ni lazima vizingatiwe katika Katiba, jambo ambali alikufanyika katika Katiba ya wakati huu. Na huduma hizo za usalama tumependekeza kwamba ni pamoja na polisi, polisi wa utawala, jeshi la ulizi, jeshi la wanamaji, jeshi la wanahewa na kikozi cha upelelezi. Tumesema vyombo hivi ni lazima vizingatiwe katika Katiba yetu.

Na tukaangalia katia ukurasa mia mbili hamsini na nane utaratibu na malengo ambayo ni lazima yafuatiwe na vikozi hivi vya huduma ambavyo ni vikozi vya kutulinda sisi kama wananchi. Na tukasema kwamba vikozi hivi havifai kufungamana na pande zozote za kisiasa ni lazima viwe na udhabiti kwa raia, ni lazima pia kutoengemea siasa za upande wowote. Tumesema pia ni lazima waheshimu kanunu za sheria, waheshimu demokrasia, waheshimu haki za kibinadamu, wawe na uwazi wa uajibikaji katika kazi yao. Waongozwe na sheria katika kazi yao na wasitii amri yoyote ambayo sio ya kisheria na wawe kazi yao muhimu ni kulinda uhuru na kusaidia wakati wa shida. Na ni lazima wawe ni watu ambao ni wazalendo na watu wa nidhamu ya juu zaidi. Na tukapendekeza kwamba Mkuu wa Polisi, Commissioner of Police awe ni mtu ambaye ana shahada ya chuo kikuu na asiweze kufanya kazi zaidi ya miaka kumi na hii miaka kumi itanganyiswa mara mbili. Kwa hivyo anaweza kufanya

kazi kwa miaka mitano ya kwanza na akakosa kuteuliwa tena lakini ikilazimika awe ni mtu mzuri asifanye kazi zaidi ya miaka kumi.

Pia jambo lingine pengine ambalo lingelitaja ni kwamba tumependekeza kubadilisha jina la gereza badala ya kuwaita Kenya Prisons tunependekeza waitwe Kenya Correctional Service na tukasema kwamba ni kwa sababu ya jukumu ambayo tunawapatia. Ukiangalia ukurasa two sixty seven, tumesema kwamba kazi yao kubwa ni kuwasaidi wahalifu kubadilika na kuwa ni watu wema na watu ambao wakirudi katika jamii wataweza kuwa na manufaa. Kwa hivyo tukasema kwa sababu ni watu ambao wanaenda kubadilisha mienendo ya watu wahalifu itakuwa bora tukitumia neno ambalo ni sawa kuliko kuiita gereza kama tunavyo ita kwa Kiswahili. Na pia tukasema kwamba kazi zao na tukazitaja ukisoma utazidi kuona tunavyo sema.

Na pia katika ukurasa wa kumi na tano tumezungumzia kuhusu the defence forces na tukatoa malengo ya kikosi hicho na kusema kwamba pia katika kikosi hicho tutakuwa na kamati itakayo simamia usalama. Na tukatoa kazi na watu watakao husika katika kukosi hicho.

Halafu katika chapter ya kumi na sita tumetoa leadership and intergrity iko katika section 276 na tumeeleza jinsi watu ambao ni wakubwa na wanatusimamia ni akina nani na pia majukumu yao ni yapi, na wametajwa hapa wamesemekana kwamba ni Rais, Waziri Mkuu, Manaibu wa Waziri Mkuu, Mawaziri, Manaibu wao, MPs, watu ambao watakuwa katika utawala wa mashinani na watu ambao watakuwa katika maofisi ya Kikatiba na mtu yoyote ambaye atakuwa katika ofisi ya umma. Na tumependekeza mambo kadhaa ambayo ni lazima wayafanye. Kwa hivyo mtaweza kusoma na kujua jinsi tutahudumiwa na watu ambao watakuwa wanashikilia kazi za umma.

Katika chapter ya kumi na sita tumeangalia vyombo ambavyo tunaviita ni vya Kikatiba. Na ukikubuka mwanzoni mwa hii draft tulisema kwamba vyombo vya Kikatiba sasa tunazipendekeza ziwe ni mkono wa nne wa serikali. Na tumependekeza Tume mbali mbali za huduma kwa mfano, Tume ya huduma ya umma, Tume ya huduma ya mahakama, Tume ya huduma ya Bunge, Tume ya vyombo vya Kikatiba na maofisa wake, Tume za Kikatiba na Tume zitakazo toa huduma za ofisini. Baada ya kuangalia hizo Tume mbali mbali za huduma tunapendekeza Tume ya Haki za Kibinadamu na kazi ambayo itafanya. Tunapendekeza kuwe na Tume ya maadili na uaminifu, Ethics and Integrity Commission itakayo hakikisha kwamba wafanyikazi wa umma na viongozi mbali mbali wanazingatia mambo ambayo tumeyaandika pale. Pia tumependekeza tuwe na Tume ya uchaguzi. Tuwe na kamati au Tume itakayo mishahara na malipo ya watu ambao wanakazi za juu za serikali kama Rais, Mawaziri, Wabunge, Ma-judge, maofisa wa kijeshi na wanatume wengine. Tumesema pia kuwe na Tume ya hazina na upunguzaji na usabasaji madaraka. Tumependekeza tuwe na Tume ya Katiba. Tuwe na, kama nilivyosema, Mkuu wa sheria, Mkurugezi wa mashtaka na kuwe na wakili wa umma ua Public Defender. Na pia tunasema kwamba watu wafuatayo watakuwa wanashikilia mamlaka ya Kikatiba kama vile Judge wakuu wa mahakama, mkuu wa sheria, governor wa Banki kuu, Auditor General. Tutakua na Tume ya ardhi. Sasa hizo ndizo Tume ambazo tunasema ama ni vyombo tunavyo sema ni Kikatina.

Halafu tukaangalia chapter ya kumi na tisa tumeiita interpretation tunaeleza jinsi ambavyo tumetumia maneno fulani.

Katika chapter ya ishirini tumeweka transitional provision ama mambo ambayo yatatuwezesha kutoka katika Katiba mzee kuelekea Katiba mpya. Halafu hatimaye tumewapa hizi orodha ya mambo tofauti first schedule tumewapa mipaka yetu na nchi jirani. Schedule ya pili tumewapa orodha ya mikoa tofauti, district tofauti na kuwapa majina yake. Schedule ya tatu tumeandika vyomba ambavyo tumesahii ni vyombo vya kitaifa. Schedule ya nne tumewapa vihapo tofauti vitavyo chukuliwa na watu watakao kuwa ni wakuu katika serikali. Halafu katika schedule ya sita tumetoa orodha ya vitu ambavyo vinafaa kutekelezwa na Bunge baada ya kupitishwa kwa Katiba hii ili kuidhinisha kwamba sheria zote na mambo yote yatakayo fanyika katika serikali yameabatana na Katiba mpya. Kwa mfano ukiangalia utaona tumesema kwamba hii hali ya kila mwananchi kupata maneno itatekelezwa kwa miezi tisa na kwamba kutokuingia kwa nchi yetu kwa watu wasio stahili kulingana na Katiba mpya jambo hili litatekelezwa kwa muda wa mwaka mmoja, sheria zinazofaa zinafaa kuandikwa. Ukiangalia kuhusu mashamba baada ya miaka miwili. Mambo ya akina mama yatekelezwe baada ya miaka mitatu. Mambo ya uraia hatukutoa muda tumesema mambo hayo yanazidi kuendelea kila wakati kwa hivyo kutolewe sheria itakayo tekeleza mambo hayo.

Halafu katika schedule ya saba tunawapatia muongozo wa utaratibu wa serikali za mashinani. Schedule ya mwisho tumewaeleza jinsi utawala utakavyo badilika kutoka Katiba ya zamani hadi Katiba mpya mtasoma na kuelewa zaidi. Sasa kwa kifupi hiyo ndio Katiba ambayo tunaipendekeza. Sisemi nimewaleza kwa kirefu lakini tulitaka tu tuwapitishe ili, na nyinyi mzidi kusoma kwa wiki ambazo zimesalia ili muone mambao ambayo mngetaka kuyapendekeza katika kikao cha kitaifa.

Na kufikia hapo nadhani kwa sababu kikao hiki sio kikao cha Tume peke yake ni kikao cha Tume pamoja na nyinyi tutawapa nafasi ya kusema ikiwa mna maneno mnataka kusema ama kuuliza swali linalo husika na hiyo document ili niweze kufafanua ikiwa amukuelewa. Asanteni na tunawakaribisha kuzungumza tafadhali ukiwa una jambo utakuja hapa mbele na kuweza kutoa jina lako na kuzungumza kwenye microphone ili tuweze kunasa sauti yako. Asanteni.

Kuna maneno ama mmetosheka? Yes mzee kuja hapa mbele na ukimaliza utaenda pale Bwana Mukewa ameketi uandike jina lako.

**Joseph Kavinya**: Asante sana kwa jina ninaitwa Joseph Kavivya Ngunzi. Langu ni swali kuhusu upande wa kamati ya utawala wa masilahi yaani kuhusu adminstration. Maana nimesikia itakuwa kuna kamati ya kuchaguliwa kuhusu administration na hatuja jua itachukua muda ngani wa kuchagua.

Pili, ikiwa inachaguliwa kupitia kuenda na kufikia location itakuwa imeweza kupatiwa uwezo wa kukaa na askari kama siku hizi kwa Katiba hii ya zamani. Chief anakaa na askali wa kulinada raia ambao hawajiwezi wakifanyiwa vibaya na wahalifu. Sasa hii itakuwa na uwezo huo ama kitakuwa namna ngani?

Ile ingine ni kuhusu hawa wanaitwa watumishi kwa serikali kama vile unasema Army, Polisi na pia Askali Kanga watakuwa ni wakati ngani watakao kaa katika ofisini mwao kama vile siku hizi watumishi wanakaa kwa miaka hamsini na tano. Yangu ni hayo na yale mengine yangu na sikuona katika maandishi haya. Ninaweza kuweka tena katika hii Committee ya kutuakilisha kwa kikao cha taifa – national yangu ni hayo.

**Paul Kyule Mutunga:** Kwa jina naitwa Paul Kyule Mutunga kutoka Iwani Location, Kaiti division, Makueni district. Ile mimi nataka kuzungumza ni upande wa wafanyi kazi wa ma-chief kwa maana nimesikia tutakuwa tukichagua watu huku katika village hili wawe wakisimamia katika kijiji. Na hapo katika location tutakuwa vile vile tukichagua watu wawili mmoja wanaume na mwengine mwanamke. Na hawa ndio watakuwa wakisimamia katika location. Na kama nikiona hapo utawala ni utawala na hapo labda mimi ninafikiria patakuwa mambo fulani kwa maana kama mtu akiwa ni mtawala anapewa uwezo wa kuongoza akiwa chief au akiwa sub-chief. Na hapo mimi ninaona hiyo inaweza kuangaliwa sawa sawa kwa maana kama akipewa huo uwezo hule atachaguliwa hapa itakuwa vizuri lakini kama hakupewa uwezo itakuwa vigumu.

Ile ingine mimi ninataka kuzungumzia ni ile tulisema upande wa kuchagua Rais. Kama Rais tukimchague na labda hana uwezo mwengine na uwezo mwengine ukipewa Waziri Mkuu, akipatiwa na uongozi mchache hiyo inaonyesha yeye hatakuwa na nguvu za kutosha kuongoza Kenya.

Na ile ingine mimi nataka kusema ni juu ya Ministers wapatiwe jukumu kama wanataka kuchukua ile inaitwa nominated members Wakenya wakikutana mimi ninafikiri watachagua yule mtu ambaye anaweza kuongaza.

Ile ingine ni ya wanawake kupewa uwezo kama mtu akiwa na brothers mali yake inaweza kungawanyiwa hao wanawake kwa vile mimi ninaona hivyo ni vizuri kwa maana mtoto, mwanamke, mwanaume wote wako sawa hata hao wanawake ndio wanasaidia wazazi kuliko hao watoto wa kiuma. Asante sana mimi nitafika hapo.

**Martin Solo:** Asante. Mimi naitwa Martin Solo Mathiva. Jambo la kwanza ni kuhusu huu utawala wa village adminstation. Vile nimeuona uenda ikawa ni Majimbo madogo kulingana na vile nimeelewa kwa sababu – sijaona serikali ya Majimbo lakini kama village itakuwa ikiji-organise yenyewe na kufanya mambo yake yake bila kuingiliwa inaonekana ni kana sort of mimi ninaona Majimbo yameingia hio kidogo.

Kuna jambo lingine ambalo sikufuraia katika huo utawala nalo ni hatujafafanuliwa ni muongozo ngani hao watu watakuwa wakifuata wale watakao kuwa wakiongoza hiyo village.

Pili, hizo village vile za sasa azijangawanywa vilivyo nafikiria kunaweza kuwa na partition ingine mpya ndio ziwe zinaweza kubana na mahitaji ya kisasa. Kwa sababu zile zilikuwa zimengawanywa zamani azijafuatilia mambo yale muhimu yote ya familia

hizo kwa sababu familia zimengawanywa mara mbili na mambo kama hayo. Pia katika tuseme tulifikiria kila Mkenya ako na haki ya kufanya kazi ya aina yoyote ile. Na hivyo sijaona Katiba ikieleza vizuri ikiakikishia kila Mkenya kwamba kuna kazi ambayo anastahili kufanya kwa sababu hule ushuru ambao wale wameajiriwa na serikali ama private sector unakatwa innakatwa kwa kila mtu. Kwa hivyo kila mtu ana haki ya kufanya kazi kiasi fulani. Hapo sijaona wakieleza vilivyo

Upande mwengine ni tumesema tunastahili kutunza misitu na mali ingine asili lakini kuna wanyama ambao wako hata huku mwetu sasa. Nafikiria wanyama wa nunga wanasitahili kukaa katiak bunga na wanadamu wakae mahali kwingine ndio hata domestic tourism iwe inaweza kuendelea. Kwa hivyo mimi kwa maoni yangu wale wanyama ambao wako katika hizi reserved areas za serikali ambazo sio bunga hawastahili kuwa huko kwa sababu wakiingia huko sasa wanaanza kututesa na sisi ni kama binadamu sasa anapoteza dhamana. Yeye mambo yake hayaangaliwi sana kuliko yale ya wanyama hao. Kwa hivyo wanyama hao wanasitahili kuchukuliwa na kupelekwa mahali ambapo wanastahili ndio tuende kuwaona huko. Nafikiria sina lingine lakini likija nitawajulisha baadaye. Asante.

**John K. Kiseve:** Kwa majina naitwa John K. Kiseve na mimi ninatoka Kaiti division, Kilala location. Mambo yenye nataka kusema ni yale nimesikia hili jambo ya wanawake au wasichana hapo kuna jambo moja alikuingia vizuri pengine ni kwangu au ni kwa wote. Kwa sababu msichana anaweza kuolewe na akiwa kwa bwana yake anarudia mali ya baba yake. Hiyo ingaliwe, tusije tukaambiwa wanawake wapewe haki. Kwa sababu anaweza kuolewa na arudi achukue mali na arudi kwa bwana yake. Anawawacha ndugu zake wakiwa hawana chochote hiyo sio sawa sawa.

Kuna kwa hii gazeti kuna kitu kimoja ambacho niliona pengine – sijue kimeondolewa ua kimebaki. Mashujaa kama Kenyatta day ikiondolewa hilo jina iwe hakuna Kenyatta day iitwe jina lingine kama vile ninasikia magereza yanabadilisha jina tutakuwa tumepota. Kwa sababu Kenyatta day ni mahali tukipotoka. Ninataka ibaki Kenyatta day na mashujaa wake kwa sababu Kenyatta hakuwa peke yake. Haya mengine yakipunguzwa hata hakuna neno.

Kuna lingine linasema wananchi wasaidie serikali na sikusikia kitu mnampa ule mwananchi wa kuwaida. Hii Katiba iangaliwe, yule mwananchi wa kawaida kabisa yule yuko chini kabisa ambaye afanyi kazi na anaambiwa asaidie serikali aangaliwe pia na yeye apate kitu. Asanteni sana.

**Gregory Mutuku:** Kwa majina naitwa Gregory Mutuku. Langu ni kuhusu Waziri Mkuu kwa vile tumeelezewa kuhusu Rais ambaye ataweza kutawala kwa vipindi viwili vya miaka mitano mitano lakini kwa Waziri Mkuu hatujafafanuliwa kama atakaa muda ngani katika utawala ama kama term yake ya utawala ni limited. Kwa hivyo mnaweza kufafanua hapo kuelezea Wakenya vile Waziri Mkuu ataweza kukaa kwa ofisini kipindi cha miaka mingapi. Asante.

**Joseph Muthembwa:** Asante sana Commissioner. Kwa jina naitwa Joseph Muthembwa kutoka hapa Kaiti. On the national days siku za kitaifa nina pendekeza hii sherehe ya Madaraka day na Jamhuri day tuwe tunazingatia hasa ku-highlight na

ku-capture freedom fighters, heros of Kenya, wale mashujaa ambao walipabania uhuru. Na ningependekeza isiwe Kenyatta peke yake kwa sababu walikuwa wengi Commission itafute jina nzuri kama heros day, freedom fighters day, jambo kama hilo nafikiri litatosha. Kwa maoni yangu Commission sioni justification ya kuwa na Katiba day sioni justification whosoever because this Constitution is subject to amendment from time to time itakuwa inabadilishwa mara kwa mara na kwa hivyo kuwa na Katiba day sijui ni hile day ambayo hii new itakua inaugurated ama itakuwa ni siku ngani kwa hivyo I don't see the justification perhaps the Commission needs to come with such justification.

On the national symbols wananchi tuko kifungu cha kumi na moja national symbols of the republic of Kenya shall consist of the national flag, the national anthem and the court of arms. Ningependekeza the court of arm iwe the only picture on our currency, pesa yetu ambayo tunatumia. Badala ya kuwa na huyu Rais picture yake akitoka tunakuwa na mwingine na yeye anaingiza picture yake hapo, mwingine akiingia ama Prime Minister akiingia anaweka picture yake hapo. I want to propose tuwe na just the court of arms kama our national symbols reflected on our currency.

Kuna sehemu ingine ambayo ningependekeza I was much interested as we were going through the Constitution the draft. Ni masilahi ya wazee, rights of wazee akina mama wale wazee, akina mama ambao hawana mapato yote. Ni kweli katika hii draft inasema wawe wanaangaliwa lakini wakati tulikuwa hapa tulipendekeza kuwe na specific allowance Commission itoe pesa kiasi fulani cha wazee akina mama na akina baba ambao hawana mapato na iwe specific kwa Katiba. Wawe wanajiangalia na wawe wanaweza kula vizuri na kuenda hospitali vizuri na kadhalika.

Pia tulipendekeza wawe wanafunzi ambao wanamaliza shule ambao hawana kazi probably from the Ministry of Culture and Social Services wawe na allowances. School leavers wawe na allowances kutoka kwa serikali kuwajali masilahi yao mpaka wanapopata kazi and that is computerized. So that kijana akimaliza shule na kumaliza shule ni kuenda mpaka training lakini hana kazi. Apatiwe kitu kidogo cha kumkalisha, akipata kazi kinaondolewa kinaanza kusaidia wengine.

We also raised the issue of pensions na hiyo sikuiona wakati tulipokuwa tunazingatia Katiba. Pension iwe specific unajua hao wazee ambao tumezungumzia sasa hivi most of them are pensioner na wengine yao ni static kabisa pengine ni mia tatu kwa mwezi hicho ni kitu kidogo sana. I want to propose to the Commission wapendekeze hiyo katika Katiba pension za wazee ziwe ninaabatana na garama za maisha. Should be adjusted from time to time according to their qualifications like an increament like those in the civil service wale ambao wanafanya kazi si wanaongezwa mishahara kila mwaka nao pensioners wawe wanaongezwa pension mara kwa mara ndipo iwe commensurate to the cost of living. Nafikiri nitakoma hapo, asanteni.

**Bonface Kitheka**: Asante sana Commissioner. Kwa jina naitwa Bonface Kitheka kutoka Kaiti, Ukia location. Kile kitu nilikuwa nataka kuzungumza ni hii mambo ya kuhusu usimamizi wa village, location, district na province. Hasa sana katika village ilisemekana kuwe na wasimamizi wawili mmoja awe mwanaume na mmoja awe mwanamke. Huu usimamizi wa mwanamke unatatizika sielewi ni mwanamke ambaye ameolewa ama ni mwanamke ambaye ajaolewa hiyo iangaliwe

isemekane vizuri. Kwa sababu mwanamke anaweza akachaguliwa akasimamia village fulani na ikawa ile tabia ama desturi ya pale haiabatani na mahali pake atakapo enda tena. Kwa hivyo hiyo ningetaka iangaliwe sana ionekane itakuwa namna ngani. Halafu tukitoka hapa location inafanya kazi pamoja na village lakini kutoka district kuenda province mimi nilikuwa naonelea haya mambo ya province yaangaliwe sana kwa sababu sielewi hasa ni kazi ngani ile itakuwa ikifanya ambayo haitashia katika district. Kwa hivyo yangu ni hayo, asante.

**Joseph Kavivya:** Nasema ni sorry kwa sababu nimesahau mengine na ninawaomba pole. Mimi pia ni mmoja wa mmoja wa Kanu na kiongozi wa vijana nikisaidiana na upande wa serikali ya chini. Kwa sasa upande huu nasaidiana na chief nikiwa hapo kama wa chama kinacho tawala. Sasa nimesikia uwezo wa vyama na viko katika Katiba. Kile chama kitakacho faulu kuwa na wajumbe wengi na kuwa na President kitakuwa na uwezo kama huu wa chama cha KANU kuwa kina ushukani na serikali kikiwa na ma-youths ama ni haje?

**Com.Abida Ali**: Nadhani tumemaliza maswali na ingefaa tuyajibu sasa.

**Joseph Muthembwa**: One more point na ninaomba radhi kwa kuwarudisha nyuma. Hizi village governments na locational governments na district governments I think the Commission should, curb napendekeza Tume ya Kurekebisha Katiba iwe very specific kuhusu kiwango cha elimu cha hawa ambao watakuwa wanachaguliwa huko na umri. Kuna mtu ambaye ametaja umri lakini ni akina nani wasiwe ni watoto, wasiwe ni wazee wakongwe. And then it says a particularly on village governments inasemekana watu waketi ni akina nani iwe specific ni hasa hasa ni akina nani ambao watakuwa wakutane waamue ikiwa ni wazee ama itakuwa kwa kupigia kura. Is it registered voters or just adults, or is it just the residents adults in that particular area. Thank you.

**Com. Abida Ali**: Asante, yes

**Stanley Kilau:** My names are Stanley Kilau from Kaiti. I am on village government tumeona representation ya governance ni women and others who are not specified. Kwa opinion yangu nimeona disabled wangekuwa included in that governance role ndio wawe wanajisema mambo yao na kuongea mambo ya wale wengine.

Ile ingine nimeonelea ni kungekuwa inclusion of youths in the governance and that member has attained the age that qualifies him not be called a youth at least kuwa member of the governance council from the village to the province and national.

Ile ingine ni on citizenship, tumeonelea ya kwamba watu wanakuja kama refugees and when they are in the country in one way or another their parents might die and they remain ambiguous in the country. --- I found that there are Commissions like Teachers Service Commission, Public Service Commission which deals only on public servants. But the Constitution is silent on bargaining power of the servant. Suppose one time the government might be in the upper hand of frustrating the rights of an

employee and there is no voice to determine which is which  who is wrong or right. So  in the  a bargaining power of public servant to me I find the Constitutiion is silent.  Thank Commissioner and the public.

**Rev. Solomon Mbusya:** My names are Reverend Solomon Mbunze and what I would like to address, there is one point where it says the mother and the father are entitled to support the child whether they are together or separated.  So my quesition here as per the old Constitution it has been appearing that when  these people separate is the man who suffers he is entitled to provide something may be to the lady and also to the childred until they attain the age of  eighteen. My question is what of the woman if she is working and may be she is the one who is  in peoblems  and has  left the man and she is not ready to provide for the childred. And I think although we are trying to promote the gender to the women you are not also looking on the men where they suffer.  That is my first question.

Secondly is on the issue of protection of the environment and natural resources. Yes we live here in rural area we have separate places where animals are kept but here we have snakes and others which damage our shambas and we would like to have these animals living the snakes, the monkeys and whatever. I don't know whether you have addressed that issue if they destroy our shambas or we even receive cases of people having snake bite and their children and they pass away, because the issue of compasation from the wild life is not all that easy.

Thirdly, I would also like to mention on the issue, it might not be well addressed I this Constitution but  I  read a paper sometimes back of a man who went and reported to the police of women having raped him and instead of the police acting they beat the man and he was chased away. That was something I read in the papers so we normally talk of women beign raped I don't know what will happen if women rape men. That is another question that I would like it  to be addressed  because it appears as if  men are always the bad people.

There is another issue of customary when we talk of the customary law and we talk of the Constitution we should also check on issues. Because if we are addressing issues, I don't know if I am a father and I would like may be my land  to be shared whether I should write a will  and say  this land should be divided according  to the customary law or according to the Constitution. Because there people are mixing some what to go to the court so that they say  let it be done according to the customary. Others want it to be done according to the Kenyan Constitution. We should specify once just as you have said that the customary laws which are pressing on women should be abolished.  I think there we should also try to strike a balance and as I finish I would say that we should do the elections using this new Constitution.  Thank you.

**Com. Abida Ali**: Thank you, I think we can now answer the questions.

**Benard Kavita:** Thank you very much.  I am Benard Kavita from Kaiti Constituency.  I want to say something on the appointees the people who wil come from every district, or province or location.  I would like the Commission to include the

youths let us have somebody representing the youths from those thirty people let us have somebody who is a youth. Because for example the youth are facing a lot of problems and sometimes we know how we can handle these problems but we have been neglected by our eleder people therefore we want to be included in decision making.

I want to say something about university degrees or university education for instance when a person get a C+ and another person get a B both of them have minmum university entrace but the one with C+ is left out and the government does not guarantee that person education in the middle level colleges. Therefore I would like to propose that the government looks into that matter. The person who gets the minimum entry marks to enter into a university be also considered. Let not the people who get Bs and above be guranteed let the person who gets a C+ and above also be guaranteed to go on with his education.

Another thing is the police. The Kenyan police are taking bribes openly when you are traveling in a vehicles they stop it and they demand for money when we are watching. We see them being given money. We want something to be done about this. And before I finish I would like the coming general elections to be held under the new Constitution. Thank you.

**Gabriel K. Manyala:** Mimi naitwa Gabriel K. Manyala kutoka hapa Kaiti division. Maneno ambayo nitasema ni mawili ama maswali. La kwanza nimeona hii Tume imefanya kazi nyingi na nzuri na ambayo hii kazi kama ninavyosoma katika magazeti hiyo kazi imechukua pesa nyingi ambazo zimefanya kazi nzuri. Na nikisoma katika magazeti hata katika radio hii kuna groups ama vikundi vya wakubwa fulani pengine wanajipendekeza kwa Rais ili hii kazi ambayo inafanywa na hii Tume isimamishwe uli uchaguzi ufanyike kwa kutumia njia ya zamani ambayo hatuipendi. Je hawa watu ambao wanajipendekeza pengine kwa Rais ili kazi nzuri iliyofanywa na hii Tume na ambayo imegarimu pesa nyingi namna hii? Hao watu wasahau hizo ndoto zao za kusimamisha hiyo nzuri mlifanya. Watasimamisha kwa njia ngani? Kwa maoni yangu mwananchi wote wa Kenya ambaye hana mambo mengine mabaya ambaye ana mafikira mazuri atafute njia y kusimamisha awa watu, ambao wanataka hii kazi isimamishwe ndio tungojee wakati mwingine, hati hii kazi yote iliyofanywa kwa muda huo mrefu, hati iwe inangojea miaka mingine. Kwa hivyo ninauliza Tume na watu wa Kenya wote muangalie hawa watu wasiharibu hii kazi ambao mmefanya. Nafika hapo, asante.

**Benjamin Kyalo:** Kwa majina naitwa Benjamin Kyalo. Kwanza ni pogezi wa wale wote ambao walitengeneza hii draft Constitution. Kitu cha kwanza ambacho ningetaka kujua ni kwa mfano, kuna pahali ambapo tunaambiwa mtu ana haki ya kukataa katika rights, una haki ya kukataa instructions which are not lawful, unlawful instructions. Sasa ningependa kujua watu wataelezwa vipi ili waweze kujua mtu akiwapatia instructions fulani wafuate, watu watajitetea vipi ili wapate kujua ya kwamba these are unlawful instructions? Kwa sababu tumeona mara nyingi wanatumia mamlaka yao ili kupata mambo fulani na vile wanawaeleza unapata anasema hivyo kwa sababu ana mamlaka fulani. Tusemi mimi nimutumie tuseme ndugu yangu mdogo kwa vile mimi ni mkubwa wake, watu wataweza kujitetea vipi especially in organisations?

Pili, ili tuangalie mambo ya elimu vijana waweze kusoma vizuri, sijui kama katika hii draft ama the main Constitution kutakuwa

na kipengele ambacho kitaonyesha vile kutakuwa na Commission fulani. Kwa sababu tukiangalia vijana wakienda kwa elimu ya juu university utapata kuna joint admission board ili kuwachukua wale ambao wana the minimum qualification to join the university. Sasa kuna wale wengine ambao wanawachwa wengi sana sasa sijui katika hii Constitution mpya kutakuwa na provision tuchukue kwa mfano wale ambao awajafikia kuenda university tuseme from B- to C+ je kutakuwa na Commission pia ambayo itaangalia maswala ya hao vijana ili waweze kupata means ya kuingia tuseme polytechinic ama other tertiary institutions ili waache kupigania hizi nafasi ambazo zimewachwa chache. That kutoka kwa C+ na C wote ili waweze kuwa na special Commission just like the university admission board ili tuweze kupunguza huu msogamano.

Sasa la mwisho kuna rights to association. Sijui kama Katiba mpya itaweza kuleta provision ya hii association imefika kiwango ngani kwa sababu tunaweza kuanza mkutano hapa katika Katiba ambayo mnayo tunayo tunafukuzwa. Nataka kujua kama hiyo right to associatio itaonyesha vitu kama demostration ama kitu kama mass action. What do we exactly mean by this assiociation. Asante.

**Com. Abida Ali**: Okay asanteni au kuna mtu mwingine nadhania tumemaliza sasa. Kulikuwa na maswali mengi kuhusu village council, district, location na provincial. Kile ningependa kusema ni kwamba tumeeleza katika chapter ya kumi jinsi ambavyo tumependekeza kuwe na utawala wa mashinani na katika pia schedule ya saba tukawaeleza jinsi ambavyo tumependekeza kazi hizo zifanywe. Lakini pengine kama nilivyo sema mwanzoni kuna mambo mengi ambayo sio kamilifu, mngeweza kufikiria zaidi kwa sababu nyinyi ndio mko mashinani na mnaelewa zaidi vile mambo yalivyo na mkapendekezo mabadiliko mkipitia wawakilishi hawa watatu ambao mtapewa majina yao pamoja na MP wa area hii kuzidi kufafanua zaidi mnavyo ona itakuwa ni vizuri kuhudumiwa. Kulikuwa na swali kama hawa village elders watapewa security nafikiria hiyo ni wazi kwa sababu hawawezi kuwa wanatawala kama awajapewa vifaa vya utawala na huduma za aina hiyo ya utawala kama huduma ya usalama.

Pia kukawa na swali kuhusu kama watawala hawa wa mashinani kweli watakuwa na authority kama ile ambayo anaye Chief. Sasa tunapendekeza kwamba tutoe Provincial Adminstration na nguvu zote zipewe watawala wa mashinani. Kwa hivyo watu wale sita hadi kumi watakao chaguliwa katiak village watakuwa na uwezo pengine uwezo mkubwa zaidi kuliko hata hule wa Chief kwa sababu chief alikuwa uwezo wake unatokana na DO na DC na sisi tumesema huo uwezo uletwe karibu na wananchi, kwa hivyo watakuwa na authority.

Na kuwa swali lingine ambalo liliuliza kwa nini kutakuwa na watu wawili. Sio watu wawili katika village au kijiji tumependekeza kuwe na watu sita na wakizidi kumi na wasipugue sita. Na hapo unaweza kusoma chapter kumi kutoka section 213 mpaka 219nna schedule seven itakueleza ni watu wangapi na watachaguliwa vipi.

Mzee yule alizungumza kwanza pia alisema kwamba hivi vikosi vya huduma vya usalama atukusema watafanya kazi mpaka kiwango ngani. Kile ningetaka kukuelezea mzee ni kwamba hii sheria kuu utoa tu miongozo na tuna sheria na kanuni za kazi

ambazo ziko kwa wakati huu na tumesema ikiwa hazikuabatana na Katiba zibadilishwe ili ziabatane na Katiba. Kwa hivyo kuna kanuni za kazi za watu wahuduma hivi vikozi vya huduma vya usalama na lazima kuna utaratibu wa vile wastaafu na atukutaka kuingilia mambo hayo, kwa sababu wananchi walipo pendekeza awakuzungumza mambo hayo na sisi atukutaka kujihuzisha nayo hasa katika Katiba.
Lakini ikiwa utaratibu wao hauabatani na Katiba itabidi Bunge ibadilishe mambo hayo.

Na pia ukaongea na kusema kwamba Rais ni lazima awe na nguvu ya kutosha ili aweze kutawala. Sasa ikiwa kama unaona nguvu za Rais zimepuguzwa sana ningekuomba ufikirie pamoja na wenzako na kuweza kutuma Wajumbe ili waje kule na kung'ang'ana kuweza kumuongezea Rais nguvu. Kwa sababu kwa wakati huu nguvu za kubadilisha hii drafi ziko kwa wananchi sio kwetu kwa sababu sisi tumefanya kazi kulingana na vile mlituambia. Mlituambia punguza nguvu za Rais pengine tumepuguza sana. Sasa mtatuma watu kule baada ya kujadiliana na mtueleze mngetaka tuongeze zile nguvu za Rais kwa kiwango ngani na tupunguze zile za Waziri Mkuu kwa kiwango ngani kwa sababu hata sasa ukunieleza umeniambia tu Rais anafaa kuwa na nguvu. Inafaa ufikirie sana na kutumana kule ili tuone tutaongeza nguvu kiasi ngani ikiwa wale delegate watakubali neno hilo.

Na pia kuna mzee ambaye amesema amefurahia sana pendekezo kwamba wasichana na akina mama waweze kurithi mali na kukaja mzee mwengine nafikiri watu wawili wakakasirika sana na hayo mambo. Kuna mzee Dominic hakufuraia hiyo na kuna mtu mwengine sasa watu wengi walitueleza kwamba wanawake na wasichana wapewe nafasi ya kurithi. Ikatubidi tufuate maoni ya watu wengi ingawaje kuna wale walifikiria kama nyinyi lakini kama nilivyosema bado kuna room ikiwa mtaweza ku-convience delegates kupitia kwa delegate wenu kwamba tubadilishe hiyo sheria tutaweza kubadilisha.

Na kuna Bwana Martini sikupata jina lake lingine akisema kwamba hii village adminstration simekaa sasa kama Jimbo ndogo ndogo. Hayo pengine ndiyo maoni ambayo unayo ikiwa hivyo ndio watu wengine wanafikiria tena mnaweza kutuma wajumbe wenu kuja na kupendekeza pengine njia nyingine ambayo mngetaka utawala uwafikie watu ikiwa upande wa village unaona tutakuwa na Majimbo ambayo ayawapendezi. Lakini ningekueleza kwamba ukiangalia chapter ten section 214 utaona kwamba tumewaeleza ama tumependekeza kwamba utawala wa mashinani ni lazima uzingatie mambo fulani. Ukiangalia 214 (1a) tumesema kwamba ni lazima utawala wa mashinani uzingatie haki za kidemokrasia na pia separation of powers na ni lazima watu hawa waajibike kwa watu ambao wamewatala na watachaguliwa na watu ambao wamejiandikisha kupiga kura. Kwa hivyo atujawapa freedom ambayo itawawezesha pengine kuwa dictators tumesema ni lazima wafuate masharti ambayo yako hapa katika Constitution, upande wa utawala. Na pia ningependa kukueleza kwamba ukiangalia section 220 inatueleza wazi kwamba district council ndiyo inatakuwa the principle level of governance. Kwamba hawa wote watakuwa wanapewa muongozo kupitia kwa district. Kwa hivyo village councils hawatakuwa wanafanya kazi bila supervision. Na pia provincial administration itakuwa mara kwa mara inawasaidia ukiangalia section 221 tumeeleza vile watakuwa wanapata usaidizi kwa upande wa utawala na upande wa kuweza kushirikiana na kuweza kufanya kazi zao kwa hali ya juu. Provincial Administration hiyo ndio itakuwa kazi yao kubwa.

Na pia Martin akasema kwamba wafanyikazi awajapewe haki ya kutosha. Ningependa uangalie section 53 ambayo inawapa wafanyi kazi haki ambayo hawana katika Katiba ya wakati huu wala sheria za nchi hii. Tumesema kwamba kila Mkenya ana haki ya kuchagua kazi apendayo na kwamba kutatolewa sheria zitakazo weza kutoa misimamo tofauti ya kikazi. Pia ukiangalia katiak bill of rights under labour relations utakuta pia kwamba wafanyikazi wamepewa haki ya hali ya juu zaidi. Section 55 tumependekeza kwamba kila mtu ana haki ya kupewa kazi inayo stahili na aweze kufanya kazi pahali ambapo panasitahili. Na wafanyikazi wote wanafaa kupewa pesa ambazo zinastahili kazi wanayo fanya na waweze kufanya kazi pahali pazuri na pia wafanyikazi tumesema wana haki ya kujiunga na chama chochote cha wafanyikazi. Wafanyikazi pia tumependekeza waweze kuwa na haki ya mgono. Kwa hivyo mapendekezo hayako katika sheria yoyote ya nchi yetu kwa wakati huu na ndio mapendekezo ambayo tumetoa kuweza kuwasaidia ama kutusaidia sisi kama wafanyikazi. Kwa hivyo ikiwa kuna mambo zaidi ungependa utaweza kupendekeza kupitia kwa delegates wa upande huu ama ukiona pengine wafanyakazi wamepewa haki nyingi ukamuelezea akazipunguze.

Halafu umezungumzia kuhusu wild life na jinsi watakavyo weza kuwekwa kado na binadamu nadhania ingawa sisi binadamu tumekosa nafasi ya kutosha ya kuishi, ukiangalia mazigara sidhani tunaweza kuwafungia na kuwaweka kado hawa wanyama kama hivyo inavyosema kwa sababu ni lazima tuangalie kwamba rasilmali ingine ya nchi ambayo tungetaka itusaidie katila maendeleo inatokana na wanyama hawa lakini tutapeleak hilo pendekezo lako mbele tuone kana kuna chochote ambacho kitafanyika. Nafikiri Bwana Dominic nimekujibu kuhusu urithi wa akina mama na vile unaofia kwamba wangechukua uridhi na kuwacha ndugu zao hawana chochote lakini mzee mwenzako alitueleza kwamba yeye maoni yake na fikira zake ni kwamba hawa wanawake ndio watu ambao wanachunga wanzao zaidi. Tulipata maoni kama hayo sana na ikatubidi kulingana na maoni tuliyopata na haki za kibinadamu na haki ambazo zimetiliwa mkataba nanchi yetu pamoja na nchi zingine za ulimwengu itatubidi tuwape akina mama haki zao, kwa sababu uwezi kusema Katiba aibagui mtu halafu upendekeza upande mwingine akina mama wanyanganywe haki zao.

Na ukapendekeza pia kuhusu Kenyatta day na umesema uoni kwa nini iondolewe, tutapendekeza hivyo na tafadhali mueleze muwakilishi wako ikiwa hayuko hapa aweze kusema jambo hilo wakati tutakuwa katika National Conference.

Haya tukaelezwa pia kwamba hatukueleza ni muda ngani Prime Minister atafanya kazi nafikiri mwenye kusema hivi akisoma kifungu mia moja na sabini na mbili atapata Jawabu Lake pale. Section 172 imesema zaidi kuhusu wakati wa kazi wa Prime Minister na tumeeleswa kwamba Prime Minister atafanya kazi mpaka wakati atakapo fakiri au akijizulu au akitolewa kwa kazi kupitia Parliament na mambo hayo matatu yasipofanyika basi ataendelea na kazi yake mpaka tutakapokuwa na uchaguzi mwingine ambapo Prime Minister mwengine atakapo chaguliwa.

Halafu kulikuwa na Bwana Joseph ambaye ameongea pia kuhusu National days na akasema kwamba haoni kwa nini tuna hiyo siku ya Katiba tutachukua hilo pendekezo lako na tafadhali mtume pia mwakilishi wako kusisitiza kuhusu Madaraka, Jamhuri

day na kuondolowe kwa Katiba day. Nafikiri hilo ni wanzo ambalo ni la muhimu.

Na pia ukatueleza kuhusu court of arms watu wengi walizungumza kuhusu currency ya Kenya na tulijadiliana kama wanatume tukaona pengine hilo jambo ambalo lingechukuliwa na sio Katiba lakini sehemu nyingine inayo hudumia masilahi ya wananchi lakini tutazidi kupendekeza mambo uliyosema.

Pia ukapendekeza kwamba wazee ni lazima wapewe allowances na watu ambao hawana mapato. Ukisoma kifungu thelathini na sita section 36 (2) inasema older members of society are entitled to reasonable care and assitance of family and the state. Kama nilivyosema Katina inatoa mwongozo kwanye Katiba atuwezi kuandika details otherwise it is going to be very bulky na tutachukua pahali pa top government policy na sheria zingine. Nafikiria tukisema reasonable care and assistance inamaanisha kwamba ni lazima waangaliwe kwa njia ya hali ya juu na kama ni marupu rupu ambayo unasema you can read in between the lines sio lazima tuseme wapewe shilingi elfu kumi we do not know the budget of the government for now. Hiyo ilikuwa sio kazi yetu kwa hivyo nadhania tulitia maanani mambo haya na tukayazingatia.

Na kuhusu watu ambao awajiweza na hawana kazi ukiangalia section 57, 59, 60 and 61 nadhania tumeweza kuzingatia masilahi yao. Section 57 tumesema kuhusu health, 59 tumezungumzia masilahi ya nyumba, 60 tukasema habari ya chakula, 61 tukaongea habari ya maji. Tunaseka serikali ihudumie wananchi wasio jiweza ukiangalia section 56 these is social security na tumependekeza kwamba mtu yoyote ambaye ajiwezi kabisa ni lazima masilahi yake na matakwa yake yatimizwe na serikali. I do not think we could have said more than that. Ukisoma tunasema every person has the right to social security including if they are unable to support themselves and their dependants appropriate social security assitance by the state. Hatuwezi kusema serikali itoe chakula, blanket sasa hiyo itakuwa tumeingilia mambo mengi. Kwa hivyo I think we have covered that.

Na pia ukazungumza kuhusu pensioners I think they are also covered under those sections na ukazunguza kuhusu mishahara ya Ministers kwamba walipwe according to their qualifications na sisi tumependekeza tuwe na Salaries and Renumeration Commission ambayo itazigatia mambo kama hayo ambayo atukuweza kuyaandika kwa urefu katika Katiba.

Bwana Boniface Kitheka alizungumza kuhusu utawala wa mashinani na akawa na wasiwasi sana kwamba tutakuwa na watu wawili kutoka kwenye village mmoja mama mmoja mwanaume na akuwa na wasi wasi na mwanaume lakini ana wasiwasi na mama. Kwanza kabisa tumesema tuwe na watu baina ya sita na kumi na matarajio ni kwamba tutakuwa na wanawake na wanaume pale ndani. Na pia uonga wako kwamba kwa nini akina mama watawekwa pale na kwamba anaweza kuwa ni msichana ama ameolewa ukisoma hii draft tumesema kuanzia section ya kwanza especially section 29 ambazo zina haki za kimsingi na ningependa tuangalie ndio watu ambao wanazidi kubagua akina mama waone kwamba mambo hayo yamekuwa ni magumu kidogo. Ukiangalia section 29 (1) tumeongea kuhusu demokrasia ukiangalia section 3 tumesema kwamba hizi haki za kimsingi ni haki ambazo ni lazima zipewe kila mtu, they belong to each individual and must guaranteed. Na kuna hii section nimeipoteza ambayo imesema kwamba hatuwezi kubagua haki ya mtu kulingana na jinsia yake, pia kulingana na status au kwa

Kiswahili sijui tutasema hali yake ya kimaisha awe ameolewe, ajaolewa ni mja mzito au wala sio mja mzito. Kwa hivyo hili jambo lako limekataliwa na wananchi wa Kenya. Kwa hivyo ikiwa mama amechaguliwa kuwa katika village council sio kisheria kama ameolewa ajaolewa awezi kukataa kuchaguliwa hapo hatufai kumbagua kwa sababu ya hali yake ya kimaisha. Na ukiangalia pia section 35 utaona kwamba sheria imekataa na inasema kwamba serikali itawapa akima mama nafasi katika gazi zote za utawala. Kwa hivyo samahani lakini jaribu bahati yako katika National Conference.

Na pia ukataka kujua kuhusu sijui kama ni wewe ama mwenzako kuhusu Provincial Council watafanya kazi ngani section 219 pamoja na schedule itakupatia kazi itakayofanywa na Provincial Council. Na mzee huyu alirudi mara ya pili kuuliza je chama kitakacho chukua usukani kutawala kitakuwa na nguvu kama chama cha KANU. Mzee sasa hapo sijui nitakujibu vioi nafikiri hayo ni mambo ya kisiasa pengine wewe ni hodari zaidi yangu kwa sababu kazi yangu siyo siasa. Lakini ninafikiria kulingana na hii Katiba vyama vya kisiasa vyote vimepewa kazi ya kufanya kwa hivyo vitafaa vifanye kazi kulingana na Katiba. Kwa hivyo tutarajie kwamba chama kitakacho kuwa kinatawa kitazingatia amri ya katiba katika kazi zake. Na pia tukaambiwa kwamba tungetoa qualificaition ya elimu na qualificaition ya miaka. Kama nilivyosema hatukutaka kuingilia sana mambo ya utawala katika mashinani, tumetoa umri wa MP, tumetoa umri wa Rais, na tukatoa kiwango cha elimu lakini tukasema katika utawala wa mashinani wananchi wenyewe wachague viongozi wao kulingana ni vile wanaona wanafaa kutawaliwa. Kwa sababu pia tulielezwa na watu wengi kwamba elimu ya darasani sio elimu peke yake. Kwa hivyo katika mashinani mnaweza kuwa na wazee walio na busara na ekima mkaona pengine watawale katika viwango hivyo. Na Provincial Adminstration katika kazi yake inafaa mara kwa mara kuwasaidia na kuwaelimisha na kuwawezesha na kuwapa uwezo.

Bwana Stanley akasema kwamba akasema kwamba Katiba katika utawala wa mashinani imesema kwamba ni wazee na akina mama Katiba ijasema wazee na akina mama hebu tuangalie. Section 14 nafikiria section ya kumi na nne imetoa muongozo ambao utafuatwa na vyombo vyote vya utawana na ikasema kwamba ni lazima wananchi wote wahusiswe kwa hivyo Katiba inatarajia kwamba watu wote walemavu, vijana ambao watasitahili pamoja na akima mama na wazee wataweza kuchaguliwa katika village council, location council, district council pamoja na Provincial Council na ndio maana hatukutoa elimu hatukusema elimu na hatukusema miaka ili tuwape watu wote nafasi. Tungesema thirty five vijana pengine wangekuja waseme thirty five ni wazee. Sasa hatukuweka tunasema watu wanao stahili kuchaguliwa wapewe hiyo nafasi.Na pia tukasema, Bunge itatoa sheria zaidi ya kuweza kusaidi katika utawala na uchaguzi wa mashinani.

Na pia kukawa na swali kuhusu Commission na kuuliza kama TSC na Public Service Commission itaweza kweli kuwasaidia wafanyikazi, nafikiri section 55 inawapa wafanyikazi wote Kenya bila kuwabagua kama ni waalimu ama ni civil servant powers ya kuweza ku-bargain na kufuata hali nzuri na pesa za kutosha za kufanyia kazi.

Reverend ingawa unasoma Standard swali lako mother and father kwamba wazee wameteseka sana katika ku-support. Mimi ninastaajabu pengine ni hapa ukambani lakini nimestaajabu Reverend kutoka kwangu kwa sababu wamama lazima wanakuja kanisani kulia kila siku kusema kwamba wazee ndio wanapata shida. Nadhani kwa kusema ukweli mama ndio uwachwa na

mtoto wazazi wakitengana. But those are your views and we will take them na sheria kama tulivyo isema sasa haijabagua imesema wazazi wote wawili ni lazima watimize jukumu. Ikiwa mama anajiweza na baba anajiweza wote wawili waungane katika kuangalia masilahi ya watoto. Na sheria ilivyo hata wakati huu ni kwamba ikiwa mama inajiweza na baba hakiwezi basi jukumu linaenda kwa mzazi anayejiweza. Sasa sheria imetoka wapi kusema ikiwa mama unajiweza usikae tu usema mzee lea mtoto sasa sheria hii imewaweka wazazi wote kwa usawa, kwamba wote wanajukumu na akina mama ambao ukimbia wakasema wewe ndiwe ulizaa chunga huyo mtoto anaambiwa sasa hauwezi kukimbia ni lazima uchunge mtoto ambaye umemzaa iwe ni ndani ya ndoa ama nje ya ndoa. Nadhani sheria hii imejaribu kutatua mambo kama hayo ambayo umeyasema.

Na ukauliza kuhusu environment na wanyama wa msituni nadhania jambo hili ikiwa pengine atukulinguzia kiwazi, pengine ni jambalo linaweza kupitiwa tena na tafadhali utume delegate wako ili aweze kuzungumza kwa sababu ni jambo ambaoli limerudiwa rudiwa na inaonekana ni jambo ambalo nila muhimu. Na ukazungumza kuhusu wanaume ambao wananajisiwa nafikiria katika haki za kibinadamu katika Katiba hii tumetoa haki ambazo ni haki ambazo zitawahusu wanawake na wanaume. Na ikiwa kuna mwanaume ambaye amekosewa na asikali polisi alipoenda kulalamika nadhania walikuwa wamekosea na sheria aijabagua.

Na pia ukazungumza kuhusu customary law na Constitution katika uridhi wa mali. Kwa wakati huu Katiba imesema kwamba sheria yoyote ikiwa imebagua mtu yoyote kinyume cha Katiba sheria hiyo haitatukima kwa hivyo sheria ambayo ni kuu ni Katiba na imeondoa ubaguzi wa aina yoyote kwa mtu yoyote.

Benard kuna kijana ambaye amekuwa na wasiwasi kwamba watu wana-qualify kuenda university hawapati nafasi ya kusoma katika shule zingine nafikiria mwenzake pia Benjamin amerudia swali hilo. Ningewaomba muangalie section 58 sub-section 3 ambayo imesema ama tumependekeza kwamba serikali ni lazima ifanye juhudi ili kuwezesha taasisi zingine za elimu ili watu wapate elimu ambayo itafaa. The state through reasonable measure shall make progressively available and accessible post secondary education. Inalazimu serikali sasa kuwapatia vijana nafasi ya kuendesha elimu yao zaidi ya shule ya upili ikiwa ni ya university, polytechnic ama elimu ya aina ingine.

Akawa pia na swali kuhusu polisi na anasema kwamba Katiba haikuzingatia corruption kwa upande wa polisi. Katiba imetueleza kwamba ni jukumu la serikali, jukumu la jamhuri ya Kenya kuondoa corruption na pia imesema ni jukumu la mwananchi kuondoa corruption. Kwa hivyo Katiba imetupatia sisi kama wananchi jukumu la kuondoa rushwa na imepatia pia serikali jukumu la kuondoa rushwa kwenye polisi na katika sector zote za serikali au sehemu ambazo kuna wafanyikazi wa umma.

Mzee Gabriel akauliza tutafanya nini na watu ambao wanazungumza na Rais na kutaka Katiba itakayo tumika iwe ni Katiba ya zamani. Mzee Gabriel ningetaka kukuhakikishia kwamba katika kazi yetu ya Tume hatukupewa kazi ya kujihuzisha na mambo ya upigaji kura, kazi yetu ilikuwa ni kutengeneza Katiba na tumeweza kuwapatia first draft hayo mengine ni siasa kwa hivyo

nitawaachia wanasiasa. ‘

Bwana Benjamin Kyalo akauliza kuhusu hii section ambayo imesema kwamba tusifuate maagizo yasiyo ya halali. Ukisoma section ya kumi na tano utaona tumeambiwa kwamba ni jukumu letu kama wananchi ya Kenya kuweza kusoma Katiba na sheria tuelewe, kwa hivyo ukiweza kuelewa sheria yako utaweza kuelewa wakati ambapo unapewa maangano ambayo sio sawa na unasitahili kukataa ikiwa umeambiwa ufanye jambo ambalo halifai.

Na ukauliza pia swali what is the limitation of the right of association? Ukiangalia section 48 and 49 itakupatia jawabu ya swali lako kikamilifu- section 48 na 49 imezungumza kuhusu right of association. Imekupatia kiwango ambacho kinawezekana section 49 imeenda na kuzungumza about assembly and demonstration na kukueleza ni demostration ngani ambayo ni peaceful na ambayo itakumbaliwa kulingana na sheria. Nadhania kufikia hapo nimejibu maswali yenu kwa uwezo ambao ninao na ninawaomba mzidi kusoma mtaelewa zaidi ya vile ambavyo tutaweza kuzungumza kwa siku ya leo na kwa kufikia hapa ningependa kuwashukuru nyote ambao mliwacha shughuli zenu na kufika hapa leo katika mkutano huu ambao ni muhimu katika historia na nchi yetu. Nimewashukuru sana na nawaomba mzidi kuzungumza na wenzenu vijiji kwenye kata na kwenye hii district yenu ili muweze kutuma watu watakao kuja na maagizo yatakayo tusaidia tuwe na sheria ya kufaa kwa siku zijazo hapa nchini. Asanteni.

**Joseph Muthembwa**: Thank you very much Commissioner kwa kunipatia nafasi ya kuuliza ni Katina nzuri kwa jumla lakini unaweza kutufafanulia ni wapi ambapo Commission imehakikisha kwamba haitavunjwa it shall not be violated and what measures shall be taken if the Constitution is violated. I am asking utufafanulie tukienda kusoma vile Commission imehakikisha ya kwamba Katiba haitafunjwa na ikivunjwa na viongozi ni hatua ngani ambayo itachukuliwa kuhakikisha Katiba hii nzuri namna hii haifunjwi hovyo hovyo.

**Com. Abida Ali**: Unajua mzee watu usema Wakenya ni wafifu wa kusoma mimi sitaki kuwasomea nataka tu muende musome it is all there. We have made provisions to ensure that you can take the steps or anybody to court when the person of the is said in violation of this Constitution. And we have said that it is the duty of every Kenyan to uphold and defend the Constitution. So you can go to court to defend this Constitution but there are provision if you take time to read the Constitution that will tell you what you can do either alone or with a group of people to ensure that this Constitution is adhered to it is all there. I am trying to get the sections for you but the sections are there if you look at chapter one section three and four enforcement of the Constitution, defense of the Constitution. So all you need is to take time to read the Draft Constitution and you will know what to do to be able to defend the document.

**Benard Kavita**: (inaudible)

**Com. Abida Ali**: You know what we have said and I have repeated here is that the Constitution cannot be so specific and we

have said from the preamble that this Constitution will respect our tradition, our diversity and our customs. I am yet know of a Kenyan tribe that says people of the same gender should marry. Is it there? It is not there although your point is right if one decided to do that then you can take them to court and say that they are violating this section of the Constitution or they are violating our --- because there are a lot of freedoms in this Constitution and rights and if you want to create mischieve you can marry another man and then go to court and said I married Kilonzo and it will be up to the court to interprete the spirit of the Constitution. And that is really not the spirit of this Constitution. I think if you read it you will be able to gather that but it is not to say that one cannot decide to be mischievous. And like wazungu wanasema the law is an act you can interprete it sometimes to suit cetain circumstances. But that really is not the spirit of the Kenyan people it is not the spirit of the Constitution.

**Nicholas Musau**: (Inaudible)

**Com. Abida Ali**: I think the coordinator will tell you the elections were done a few weeks ago. He should be able to tell but without giving you details the people who are going to be in the Conference are Members of Parliament. We are also going to have the Commissioners who will attend and have no say or vote we shall just be there to defend this document when people question. Then we are going to have three delegates from every district one of whom has to be a woman. Then we are going to have the religious community bringing a number of delegates. I don't remember the number off head of the religious organizations, I don't know whether they are thirty five. Thirty five religious leaders or people appointed by religious organizations will attend. Then we are going to have twenty four representatives of the women organizations. They we are going to have people from professional organization fifteen and there is also civil society sixteen from the trade unions and other interest groups. The Commission then will have to look at people who have been marginalized and there are thirteen slots which to the best of my knowledge have already been filled. So we are going to have six hundred and twenty nine delegates at the National Conference.

**Charles Mulei**: (Inaudible)

**Com. Abida Ali**: Yes there is a provision where the state will provide legal representation in case the sentence is going to be advanced to the accused person. So it is not every small offense but it has to be a serious offense and the state is required to provide in such circumstances legal representation. And where a child is taken before a court of law the state has an obligation to provide a child with a legal represetative. (Interjection iaudible) why don't you read you now you want me to read for you and I have said Kenyans have a culture of being lazy. Please read that document and all those things are there. You read you will find everything there. Although I don't blane they have come in today but they are all there. Is there another clarification may other than a question. Yes at the end.

**Gregory Mutuku**: I am glad that you have clarified for me about the Prime Minister though I give as a proposal for you to forward to the Commission that the period for the Prime Minster you have clarified that it is may be death of after general

election. But in a situation where for example a Prime Minister is appointed by a President from a particular party and then that particular party wins elections may be in three or so consecutive terms may be that party may decide to still be appointing that Prime Minister for that post – particular individual. Then I think it would be better if a specified period is proposed in the Constitution that, that Prime Minster will hold that office.

**Com. Abida Ali:** Thank you. We will take that but please sent your representative also to give that because for now all we are saying is that Parliament approves the appointment of a Prime Minister. Asanteni.

**Sammy Kiteng'u**: Thank you so much Commissioner. I would like to take this opportunity to close this meeting with this one suggestion that even though I am going to give you the names of the Makueni district representatives. You might find that they are too far for you please if you have any suggestion that you want them to go with you can write them and bring them to my office at Wote. And this district elected three representatives from the county council councilors on the 17th September this year. And the representatives where Rodah Ndumi Maende from Makueni Constituency, William Matheka Nduse from Kilome Constituency and Praxides Nzisa Wambua from Makueni Constituency. So those are your three district representatives. And if you find that you cannot make it to the office at Wote then your area Member of Parliament will be a delegate in the National Constitutional Conference, you can still write your proposal and give it to him for him to present it. I think with that I would ask Reverend again to pray for us to close the meeting.

**Rev. Solomon Mbunzya**: Lets pray. Our dear heavenly Father we are grateful unto thee because you have been with us thoughout as we have been going through the Constitution. And Lord we pray that even as we have the national delegates Lord Father that our views are going to the presented. And Lord the Constitution will come out clearly without any interference and Lord we have found it good and worthy being used in our country. Lord we pray that the views from the delegates will be Lord respected and they will not be interfered with. We pray for those entire Lord who will be there to answer the questions that you are going to give wisdom. Lord thank you because of being with us, because of being with the participants, because of been here infront of us to lead us especially Lord our Madam who has really done a lot she has tought a lot. We are pray that you are going to give her enough strength, you are going to give her Lord enough energy Lord as she goes round and gets peoples views that you are going to be with her and you are going to strengthn her and even provide journey mercies throughout the places that she is going to travel in. Lord us and be with us as we continue in Jesus name we pray. Amen.

Meeting closed at 2.30 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**